# *IBRAHIMU*

Hebu na tuendelee kusimama kwa muda kidogo tu. Nilisikitika kwa kuchelewa kidogo usiku wa leo, lakini nilikuwa kwenye chumba cha dharura huko nje, nami nikacheleweshwa kidogo. Kwa hiyo, kabla hatujaketi, ningetaka kusoma Maandiko hapa yanayopatikana katika Mwanzo kumalizia somo nililoanza jana jioni. Katika Mwanzo 22 tunalisoma, hili kutoka kwenye kifungu cha 7:

> *Isaka akasema na Ibrahimu baba yake, akanena, Babangu: naye akasema, Mimi hapa, mwanangu. Akasema, Tazama, moto upo, na kuni zipo, lakini yuko wapi mwana-kondoo kwa sadaka ya kuteketezwa?*
>
> *Ibrahimu akasema, Mwanangu, Mungu atajipatia mwana-kondoo kwa hiyo sadaka ya kuteketezwa: basi wakaninii*. . .*wote*. . .wakaenda *pamoja.*

2 Na kifungu cha 14 tena:

> *Ibrahimu akapaita mahali hapo Yehova-yire: kama watu wasemavyo hata leo, Katika mlima wa* B*WANA* *itapatikana.*

3 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa muda kidogo tu, tunapomwendea Mwandishi wa Neno hili katika maombi.

4 Baba mwenye rehema sana, tuna furaha usiku wa leo, ya kwamba Mungu wa Ibrahimu ndiye Mungu wetu, ya kwamba sisi tu watoto Wake kwa ile ahadi iliyo katika Yesu Kristo, basi, na Yeye ni yule yule tu usiku wa leo kwa watoto Wake, kama alivyokuwa kwa baba Ibrahimu, kwa ajili ya kile alichokuwa kwa Ibrahimu, ile baraka haikumwahidi Ibrahimu pekee, bali pia watoto wake baada yake. Na wakati Yule aliye mkuu na mwenye nguvu alipokuja, yule Mtoto mwenye nguvu, Bwana Yesu, Yeye alitolewa kwa ajili ya dhambi, kwa ajili ya dhambi zetu, ili sisi, kwa haki Yake, tupate kuwa watoto wa Ibrahimu, ambao ni watoto wa Mungu kwa ahadi.

5 Sasa, Baba, tunaomba ya kwamba utatupatia, usiku wa leo, imani aliyokuwa nayo Ibrahimu. Na tunapozungumza juu ya Neno, Roho Mtakatifu na athibitishe yote uliyoandika. Na jalia, tutakapoondoka hapa usiku wa leo, baada ya mstari huu wa maombi kwisha, tuanze kwenda kwenye makazi yetu mbalimbali, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau, "Je, mioyo yetu haikuwaka ndani yetu, hapo aliposema nasi njiani?"

6 Na afanye usiku wa leo, mambo aliyofanya kabla ya kusulubiwa Kwake, kusudi hii Emau usiku wa leo, iweze kujua ya kwamba amefufuka katika wafu, na upesi, tutaenda, tukiwaambia wengine, "Hakika, Bwana amefufuka katika wafu,

na ametutokea hapa Yakima." Tunaomba hayo, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

7 Mwaweza kuketi. Kuna wengi wanaoweka leso hapa juu, mimi huziombea kila usiku. Ninakumbuka huko Afrika Kusini, kimoja cha vitabu, naamini kiliandikwa na Kasisi wa jeshi Julius Stadsklev, aliandika kitabu, naamini, *Nabii Azuru Afrika*, nao walikuwa na magunia kadhaa makubwa ya turubai jukwaani, yaliyojaa barua, ndipo mhariri wa gazeti la *Mtangazaji*, akasema, "Ndugu Branham ni mshirikina sana." Kasema, "Alikuwa akiombea kitambaa."

8 Wao tu, kamwe hawakusikia habari zake, mnaona. Na bila shaka, hiyo ni sehemu ya Injili, hilo ni jambo ambalo Mungu ameahidi kwamba Yeye alilibariki. Nasi tuna m—msururu, maombi, kote ulimwenguni kwa ajili ya vitambaa hivi, baadhi ya watu huamka saa sita, wengine saa tisa usiku, nasi sote tunasafiri na kuomba kulingana na Mfumo wa Saa za Mashariki. Tunazituma hizo kutoka maskanini kote ulimwenguni. Watu huamka, wakiwaombea wengine, si kujiombea wenyewe, kwa ajili ya wengine, na wengine wanawaombea, kama tufanyavyo hapa usiku. Nami nawaambia, mnapaswa kuona shuhuda zinazokuja za mambo makuu aliyofanya Bwana.

9 Nikizungumza tu, jana usiku, kwenye chumba cha dharura, kulikuwa na maskini, mwanamke Mjerumani aliyetumwa si muda mrefu uliopita, naye akachukua kitambaa cha maombi, na kwenye ninii—ninii. . .Ni kipande kidogo cha utepe, nilikuwa nikituma leso, lakini walipokuwa wengi kupita kiasi, nisingeweza kufanya hivyo, kwa hiyo hununua tu mamia ya yadi za utepe, ninaketi chini nikiziombea, nawatumia wagonjwa na wanaoteseka.

10 Basi maskini mwanamke huyu Mjerumani, alipata maagizo, nao wakamfasiria jinsi yalivyokuwa huko Ujerumani, jinsi ambavyo kwanza unamwita mchungaji wako, na endapo mchungaji wako hawezi kuja, Mkristo fulani mzuri, kutoka kwenye ujirani, ama mtu wa familia yako, unaungama makosa yako yote, kama una yoyote, unaomba, unachukua kipande hiki kidogo cha nguo, na kukibandika kwenye vazi la ndani, unakiwekea mikono, na kumwambia Mungu ya kwamba utamtumikia maishani mwako mwote iwapo Yeye atakujalia upate afya.

11 Halafu basi, unapofanya hivyo, basi kila saa kwenye saa za kale za dhabihu, saa tatu, saa sita, na saa tisa alasiri, Mfumo wa Saa za Mashariki, hapo ndipo ninapoomba wakati uo huo, nasi tunaomba siku nzima namna hiyo, na kote ulimwenguni. Nawe unaninii tu. . .Mungu hawezi kuyapuuza hayo, kote ulimwenguni dakika ile ile ni maombi ya mamia na mamia ya watu yakivuma kwa wakati mmoja.

12 Basi maskini mwanamke huyu Mjerumani akaweka hicho juu yake, naye akawaita majirani zake, mchungaji wake, alikuwa na yabisi kavu kwa miaka ishirini *na kitu*, kwenye kiti cha magurudumu. Kidogo lilikuwa ni la kupendeza, na nyeti, lakini alisema, alipokiweka hicho pale alisema, "Sasa, Bw. Ibilisi, huwezi kunishikilia tena, kwa hiyo toka tu, mimi hapa naja." Akatoka kwenye kiti cha magurudumu, na akaanza kutembea. Naam. Rahisi tu hivyo, ni rahisi tu jinsi hiyo, imani ni rahisi.

13 Na sababu ya mimi kuchukua siku hizi usiku, kuzungumza juu ya imani, ni kwa sababu watu wanajaribu kuifanya imani kuwa ngumu. Mungu haifanyi ngumu, sisi ndio tunaoifanya ngumu. Tunaenda huko mbali sana, tukijaribu kupata kitu fulani huko nje, na hiki hapa papa hapa karibu nasi, rahisi. Kama una imani ya kutosha kutembea kwenye sakafu hiyo, una imani ya kutosha kwa chochote Mungu alichoahidi. Kama una imani ya kutosha kuinua mkono wako, mbona, u—una imani ya kutosha kwa kitu kingine chochote. Ni imani rahisi. Ipake tu kwa hisopo, ambayo nimewaambia katika jumbe.

14 Chukua tu Damu na kwa imani rahisi, kama tu vile unavyokula, kunywa, kutembea, kuendesha gari lako, kuzungumza, ama chochote kile, ni rahisi tu hivyo. Lakini wakati, unapoanza kuwazia, "Loo, naweza kufanya hivyo? Naweza kufanya hivyo?" Unaona? Ndipo una—unaenda moja kwa moja mbali na—na jambo muhimu. Unapaswa kurudi hapa kwenye imani rahisi, kama ya mtoto, kumwamini tu Mungu, useme, "Mungu aliiahidi, mali yangu, Kristo aliifia, nayo ni yangu," na uendelee tu moja kwa moja, na kuamini, wala usiwazie kitu kingine kulihusu, ninii tu, ni sawa, yote yamekwisha, nawe utapona. Sasa, ninajua hiyo ni kweli, kwa sababu nimeijaribu.

15 Lakini sasa, kama una dhambi isiyotubiwa moyoni mwako, hakika haitafanya kazi, inakubidi kukiri dhambi yako. Mwamini Bwana Yesu Kristo, mkubali Yeye kama Mponyaji wako, kama tu vile ungefanya kama Mwokozi wako.

Wanasema, "Hivi—hivi uponyaji wa Kiungu hudumu, Ndugu Branham?"

16 Maadamu tu imani inadumu. Unapofikia mahali ambapo unasema kwamba hujaokoka tena, kumbuka, umepoteza mahali pako papo hapo. Maungamo yako yakishuka, basi imani yako inashuka.

17 Na sasa, jambo la kwanza ambalo Waebrania husema hivi, kwamba Yesu Kristo ni Kuhani Mkuu anayetuombea tunapokiri. Na kabla Mungu hajakufanyia jambo moja, inakubidi kwanza, kukiri kwamba amelifanya. Yeye ni Kuhani Mkuu wa ninii yetu. . .Bila shaka, la King James linasema kuungama, na *kuungama* na *kukiri* ni neno lile lile. Mnaona? *Kuungama* kwamba ndivyo ilivyo, ama *kukiri* kwamba Yeye ndiye. Unaona?

*Kuungama*, ninaungama mimi ni Mkristo, ama *kukiri* mimi ni Mkristo, haileti tofauti yoyote.

18 Ndipo basi, na yule mwanamke akigusa vazi Lake, ilisema, "Imani yako imekuokoa." Sasa, hawa wasomi wa Kiyunani hapa, wangekwambia, ya kwamba neno hilo hapo katika Kiyunani ni *sozo*, ambalo linamaanisha sawa kabisa na, "kuokolewa kimwili," ama "kuokolewa kiroho," vile vile katika tafsiri, *sozo*. "Imani yako imesozo," imekuokoa. Imani yako inakuokoa na kuzimu, imani yako inakuokoa na mauti, imani yako inakuokoa na magonjwa, unaona. Ni *sozo*, neno lile lile.

19 Kwa hiyo imani ile ile uliyo nayo katika Mungu kwa ajili ya wokovu wako ndiyo imani ile ile unayotumia kwa uponyaji wako. Rahisi tu, iamini, ifanyie kazi, haihitaji mihemuko yoyote, haihitaji chochote ulimwenguni ila tu imani ya kawaida. Haikubidi kuhisi chochote. Haikubidi kuninii. . .Jambo pekee likupasalo kufanya ni kuamini jambo fulani, amini ya kwamba Yesu alikufa upate kuokolewa, na ni yako. Imani ni rahisi sana.

20 Hivi majuzi, kulikuwako na ninii, nilikuwa nikitembea huku na huku, na kulikuwako na m—mhudumu ameketi chini ya mti, Roho Mtakatifu akaniambia, "Nenda ukazungumze naye." Nikaenda pale, naye mke wake akatokea, na kundi la watu waliokuwa hapa, wala wasingeweza kupata kadi ya maombi, wala hawakujua kulikuwa na chumba cha dharura, nao iliwabidi kurudi. Mnaona neema ya Mungu?

21 Ndipo basi, vema, nilipokuwa pale, Roho Mtakatifu alishuka na kuanza kufunua mambo ya kila namna. Ndipo hao watu wakaanza kulia, na kupiga makelele. Nami nikasema, "Ulikuja pamoja na Mhindi fulani. Yuko wapi?" Na kwa hiyo nikasema, "Huyo Mhindi ni msichana mdogo, naye alikuwa na homa, imepoozesha ubongo wake." Ndipo mtu huyo akaanza kulia; alikuwa mmishenari kwa Wahindi. Naye akasema. . .Nikasema, "Mlete huyo msichana, tutamwombea." Nami nikasema, "Baba yake hana pesa za kukaa usiku mwingine."

22 Hilo ndilo linaloniumiza. Sijui jinsi ilivyopata kutukia. I—i—itanibidi kuacha kufanya yale ninayofanya, kwa sababu sipati mawasiliano ya kutosha na watu hawa kupitia maono haya.

23 Watu Marekani, tumefundishwa kwa muda mrefu sana hatuna budi kuwekeana mikono. Na kwa kweli, hivyo ndivyo hasa wito wangu ulivyopaswa kufanya, Malaika wa Bwana aliniambia, nilizaliwa kuwaombea wagonjwa. Mimi ndiye niliyeuliza, ndipo Yeye akasema, "Kwa ishara hizi, itawafanya, waamini."

Nikasema, "Hawangeniamini. Sina elimu, wala hawangeniamini."

Akasema, "Kwa hii hawana budi kuamini, maana utajua mawazo yenyewe ya moyo wao."

24 Mara nyingi natamani wakati mwingine ningalikuwa na kitu kingine, kwa maana mara nyingi ninasimama mbele ya watu, wanaoweka mikono yao mgongoni mwangu, na kuniita ndugu, nami najua hilo ni kosa. Mnaona? Nimesimama pamoja na, hata na watu wanaokaa, na kusema, “Loo, Ndugu Branham, ninaye Roho Mtakatifu,” na mambo kama hayo, na kujua wanaishi na mke wa mtu mwingine, ama mume wa mwanamke mwingine. Kusimama na kumeza hilo wakati unajua tofauti, inakatakata na kuumiza. Kamwe usiitamani, usiitake kamwe, hujui kinachoambatana nayo, unaona.

25 Rafiki yangu mwema, tulikuwa tu tumeketi mezani, mhudumu, nami nilikuwa nimemwandikia, naye alikuwa ni mtu mzuri, nilikutana naye nami nilikuwa tu nimeketi mezani nikila siku moja, na huko chini Louisiana, jambo fulani likatukia. Nikaangalia upande wa pili wa meza, na laiti nisingalifanya hivyo, limeniumiza tangu wakati huo. Laiti nisingalifanya hivyo! Hiyo ndiyo sababu, ninajaribu kuiweka mbali kadiri niwezavyo, nisije nikaiona. Si—sitaki kuwa na hisia hiyo, nataka kuamini ya kwamba kuna . . . anayenipenda, kwa vyovyote vile, mnaona. Nawe hutaki kuwa nayo, wala hutambui kile kinachokubidi kupigana nacho, ukijua.

26 Halafu basi, kile mtu fulani asemacho, na kile mtu anachomaanisha moyoni mwao wakati mwingine ni mambo mawili tofauti. Na unachukia kujua hilo, kwa sababu ninawapenda watu, nami ninataka kuwapenda kwa upendo wa kweli, pasipo kujua hata wanachowazia. Lakini hilo halileti tofauti yoyote, bali na—nataka kupenda, kwa vyovyote vile. Halafu basi, lakini kadiri tunavyoweza kuwa rahisi zaidi, ndivyo tutakavyokuwa bora zaidi.

27 Nilikuwa ndio kwanza nizungumze juu ya Wahindi. Ninakumbuka mara yangu ya kwanza kuhusika na Wahindi. Nilimwahidi Bwa—Bwana, kwa mmishenari huyu, nilipomwombea yule msichana mdogo, na kumtuma nyumbani, kama . . . na kusema, “Bwana, kama Wewe utamjalia mtoto huyo apone, nitaenda risavuni.”

28 Ninakumbuka huko Phoenix, mara ya kwanza ilikuwa huko San Carlos, Waapache, Wahindi wa kwanza niliowaombea. Sikuzote niliwahurumia Wahindi, hawakupata mgawo mzuri sana, tunajua hilo. Kwa hiyo usiku huo huko San Carlos, huko nyuma miaka mingi iliyopita, walikuwa na . . . tulienda kule, nasi tukasema, “Wahindi pekee.”

29 Na kwa hiyo walikuwa huko risavuni mwao, na loo, wakati jua lilipotua alasiri hiyo, ilipendeza kuwaona nanii, wote wameketi juu ya mablanketi, na kadhalika, wanasimama na kuketi. Nami nilikuwa katika misheni ndogo ya Assembly of God huko nje barazani, mnenaji mmoja na mkalimani mmoja,

na mwanamke huyo. . .Hawana sentensi zozote, wala aya, wala vituo, mazungumzo kidogo ni makali.

30 Na kwa hiyo mimi, yeye alikuwa akifasiri, ndipo nikaendelea, na kusema, "Sasa, ninyi watu, ninawahurumia," Nikasema, "lakini mimi ni Mmarekani mmoja tu." Nikasema, "Sidhani ilikuwa sahihi, kuwasukumia huku nje katika sehemu hizi, na kadhalika," Nikasema, "Nafikiri ni moja ya madoa makubwa sana yaliyopata kuingia kwenye bendera."

31 Nami nikasema, "Tungejisikiaje kama Japani ingeshinda vile vita, na kutusukumia mahali kama hapo? Halingeonekana zuri sana. Kwa hiyo, nanyi mnaishi huku nje na TB na kadhalika, kidogo mna njaa, na kadhalika, huku tunatuma misaada ya mamilioni ng'ambo ya bahari, haya basi."

32 Mnaona, kwa hiyo kile. . .Wema wa mtu huanzia kwao, inasema Biblia. Na kwa Mmarekani halisi. . .Kumbukeni, sisi si Wamarekani, wao ndio, Mungu aliwapa nchi hii, tuliwavamia, tukawanyang'anya kwa nguvu, tukawasukumia jangwani mahali fulani, katika nchi maskini sana. Kwa hiyo hivyo ndivyo. . .Tunawapa malipo kidogo ya uzeeni, ama *kitu kama hicho*, karibu ya kutosha kumlisha mtoto mmoja, nami sikuzote niliwasikitikia, nyanya yangu alipata malipo ya uzeeni.

33 Kwa hiyo basi mimi, huko nje usiku huo. . .Mhindi ni mtu wa ajabu, yeye ni kama nyumbu, hatakula kutoka kwenye zizi la mwingine, kwa hiyo a—aliketi pale na kuangalia huku na huku kwa muda, nawe ungeweza kuwaona wameinamisha vichwa. Yeye atasimama na kukusikiliza, bali hutajua au kuwazia anakusikiliza, bali anashika kila neno unalosema.

34 Kwa hiyo, wakati ibada, nilipomaliza kuzungumza, nilisema, "Sasa, nimekuja kuwajulisha Mtu atakayewapa haki, huyo ni Yesu Kristo," nikasema, "Yeye anawapenda, nami nipo hapa kumwakilisha. Serikali, na kadhalika, inaweza kuliwakilisha taifa, bali mimi," nikasema, "nimekuja hapa kumwakilisha Yeye, Naye atawapa haki."

35 Ndipo basi, nilipomaliza kusema hivyo, nikasema, "Sasa, wote wanaotaka kuombewa. . ." Hakuna haja, usingeweza kuwapa kadi za maombi, maana hapakuwapo na njia ya kuwapangisha mstari, inakubidi tu kushikilia mahali padogo hapa, na kumwacha mmoja apite apendavyo. Kwa hiyo, nikasema, "Sasa, ninyi nyote mnaotaka kuombewa, simameni."

36 Vema, nilikuwa nimeondoka huko Phoenix pamoja na Wahispania, na loo, jamani, li—lilikuwa ni jambo la kuchukiza sana, wao, jinsi wangekuja mstarini, maelfu yao. Ndipo basi, nikasema, "Sasa, jambo hilo. . ." Nikasema. . .Nami nikaangalia, na nikafikiri kila mtu angeruka juu na kukimbia, lakini hakuna mtu aliyeruka na kukimbia, kila mtu alikaa kimya. Nikasema, "Je, ulisema niliyosema?"

Akasema, "Naam, bwana."

37 Nikasema, "Sema tena." Nikasema, "Kila mtu anayetaka kuombewa, apande vipandio upande *huu*, kisha avuke upande *huu*, kwa imani akimwamini Yesu Kristo, yale nimewaambia."

38 Na kwa hiyo, hakuna mtu aliyesimama, kila mtu alitulia tu kikamilifu kabisa, hakuna mtu aliyesimama hata kidogo. Basi baada ya kitambo kidogo huyo mmishenari akarudi chumbani, na kumleta mwanamke Mhindi. Vema, nikageuka, nikaangalia nyuma yangu, ambalo sikuwa nimeangalia bado, nao walikuwa na watoto hawa wote wachanga kwenye maskini mifuko hii waliyo nayo mgongoni mwao, mwajua, imetundikwa ukutani, kulikuwa na kundi la wanawake mle ndani.

39 Huyu hapa mwanamke mmoja anakuja, mwajua, akiwa na maskini mtoto huyu mchanga, akaniangalia, nami nikasema, "Ninaweza kuushika mkono wako?" Na kifundo kikubwa mno, kipana, cha mkono, naye akaniangalia kidogo, nami nikamwangalia, kisha nikasema, "Sasa, mwanamke huyu anaugua kifua kikuu, naye ana glakoma ya jicho, pia."

Naye mkalimani akasema hivyo, naye akageuka, akaniangalia, "Ulijuaje hilo?"

40 Nikamwombea. Mwingine aliyepitia, si kwa sababu ya maisha machafu, bali jinsi ilivyombidi kuishi, alikuwa na ugonjwa wa zinaa, mchafu, bali si kwa maisha machafu. Kisha nikamwambia. . .Naye akaniangalia, na hao Wahindi wote walikuwa wakitazamana.

41 Aliyefuata alikuwa ni msichana mdogo, naye mama alikuwa pamoja naye, na kwa hiyo nikasema, "Maskini huyu msichana alikuwa na homa, nayo hiyo homa ikamfanya kuwa kiziwi, hawezi kuzungumza wala kusikia, yeye ni bubu."

Basi mkalimani alipomwambia huyo mama hivyo, mama alitikisa kichwa chake, "Ndivyo."

42 Na—naye baba yake alikuwa mmoja wa hao machifu, nami nikamchukua maskini msichana huyo mikononi mwangu, na kumwombea huyo mtoto. Maskini nywele zake ngumu kama manyoya ya farasi, mwajua. Kwa hiyo, nikamwombea, na kumweka chini namna hiyo. Nikasema, "Angalia hapa, mpenzi." Nikasema, "Unanisikia?" Nikakigeuza kichwa chake namna hiyo, mwajua, nami [Ndugu Branham anapiga makofi—Mh.] nikafanya hivyo. Akaangalia kote, yeye, hayo macho madogo meusi, yakaniangalia. Nikasema, "Anaweza kusikia, nami nina hakika anaweza kuzungumza."

Akasema, "Blee blah blah," *kitu fulani* namna hiyo.

"Loo," nikasema, "atazungumza vizuri kuliko hivyo."

Mkalimani akasema, "Mazungumzo yake ni mazuri sasa." Kwa hiyo alikuwa tayari kuninii. . .vema.

43 Kwa hiyo, basi aliyefuata alikuwa ni mvulana mdogo, mwenye makengeza. Ndipo Wahindi wakaanza kuangalia.

Mwingine akajitokeza, alikuwa ameinamisha kichwa chake, kidogo kimerudi nyuma, maskini mashavu yake manene ya Kiapache yameinama, nywele zikining'inia machoni mwake. Nami nikasema, "Sasa, maskini huyo mvulana, ndiye mvulana anayetaka kuombewa?"

Naye mkalimani akasema, "Mama, naam."

44 Nami nikasema, "Sasa, mvulana huyu mdogo ana makengeza." Na kwa hiyo, Hiyo ikasema hivyo, ndipo huyo mama akaunyosha mkono huo, mara akashika nywele za kichwani, na kumvuta nyuma, nayo maskini macho yake yamekaa namna *hiyo*.

45 Basi nikasema, "Hebu nipe huyo mvulana mdogo." Nami nilikuwa na kipande cha chingamu mfukoni mwangu, nikampa, naye akaishika, akanitazama kwa mshangao. Nikamchukua mikononi mwangu, nami nikawazia. . .nikasema, "Usifasiri hili."

46 Nikasema, "Baba wa Mbinguni, naomba unipe neema. . . " [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] " . . .machoni—machoni pa watu, ili niweze kuwaongoza hawa Wamarekani halisi Kwako," Nikasema, "kwa Roho Mtakatifu, kitu ambacho kitawapa amani, na—na kuwapeleka nyumbani Utukufuni. Macho ya mtoto huyu na yafunguke. Ninamwamuru Shetani amwachilie."

47 Nikaangalia mbele yangu, nikaona ono la huyo mvulana mdogo akiniangalia moja kwa moja, *hivi*, na macho yake yakiwa sawa kabisa. Hao Wahindi, walikuwa wameketi tu, wakiangalia. Ndipo basi nikasema, "Sasa, kabla sijamgeuza huyu mvulana mdogo," alikuwa amelaza kichwa chake begani mwangu, "kama macho ya mtoto huyu mchanga hayajanyoka basi mimi ni nabii wa uongo, nifukuzeni humu risavuni. Kama yamenyoka, ni wangapi watampokea Bwana Yesu?" Wote wakainua mikono yao. Nikasema, "Unaonaje, mama?" Kwa huyo mwanamke namna hiyo.

Naye akamnong'onezea mkalimani kitu fulani, kasema, "Alisema, 'Kama angeweza. . .Kama Mungu angeweza kuponya viziwi na bubu, angeweza kuyanyosha macho."

48 Hiyo ni falsafa nzuri, hiyo. Kwa hiyo nikamgeuza maskini huyo mvulana, macho yake yalikuwa manyofu kama yangu. Loo, jamani, mwanena kuhusu mstari wa maombi? Tulikuwa na mkurupuko, walikuwa tu wakija kila mahali. Ndipo nikamwuliza mkalimani, kasema, "Walidhani kwanza ulikuwa mwongo, lakini sasa wanajua ya kwamba ni kweli."

49 Jambo moja tu zaidi, kulikuwako na Ndugu Jack Moore. . . Ni wangapi waliopata kumjua Ndugu Jack Moore, ninyi wahudumu, kutoka Shreveport, Louisiana? Alikuwa mmoja wa Wafanyabiashara Wakristo. Mnamjua. . .?. . .na labda wengi wenu, huko nje, mnamjua Ndugu Jack Moore kutoka Shreveport.

Naam, angalieni hiyo mikono. Alikuwa pamoja nami, yeye na Ndugu Brown.

50 Na kulikuwako na mama m—mkongwe wa Kihindi aliyekuwa wa pili mstarini kutoka hapa, lakini kulikuwako na mvulana mdogo wa Kihindi, yapata umri wa miaka kumi na minane, jamaa mdogo, mnene, alijisukumiza tu moja kwa moja ndani karibu na hao wengine. Nami nilikuwa na mstari wa maombi moja kwa moja mpaka San Carlos, wote—wote wamejipanga tu pale, kila mtu alitaka kuombewa. Kwa hiyo ni—nisingeweza kumfanya huyo mvulana mdogo arudi, wala mkalimani asingeweza kumfanya arudi. Kwa hiyo, yule mwanamke mkongwe kweli ndiye aliyefuata, naye Ndugu Jack ndio kwanza amshike mikono, Ndugu Jack ni mnene sana, mtu mfupi, akamnyanyua tu na kumrudisha nyuma.

51 Vema, aliyefuata alikuwa ni mwanamke mzee Mhindi, alionekana kuwa na umri wa kama miaka sabini na mitano, akiwa na vijiti vya fagio vilivyokatwa vikawa mikongojo, huku matambara yamezungushiwa kijiti kilichopita juu ya sehemu iliyopitia juu ya mkono wake, naye alikuwa amejishika *hivi* mlangoni. Basi nikamwashiria, naye akanyosha kijiti kimoja namna *hiyo*, na kusogeza mguu wake, kisha huo mwingine. Nilichukua tu wakati wangu, nikamngojea.

52 Naye akakaribia mahali nilipokuwa, nami nikawazia, "Huyu bikizee atafanya nini?" Ndipo nikaona nywele zake zimening'inia chini, zimesokotwa kwa ngozi, mwajua, na zinaingia mvi. Nikawazia, "Maskini kizee, labda alilea kundi la watoto. Ni huzuni jinsi gani! Laiti ningaliweza kuzungumza lugha yake."

53 Naye akaniangalia namna *hiyo*, na hayo macho madogo sana, yaliyoingia ndani, kidogo yamefifia rangi, makunyanzi makubwa mno mashavuni, nayo machozi yanatiririka kupitia makunyanzi hayo. Loo, moyo wangu ulimhurumia tu maskini huyo bikizee! Naye akaniangalia namna hiyo, kidogo akatabasamu, akanyosha mkono na kuchukua mkongojo mmoja na kuuweka kwenye huo mkono mwingine, akanikabidhi hiyo, kisha akaondoka jukwaani akitembea kama tu mtu mwingine yeyote. Mnaona? Sasa, nawaambia, naam, hakuna maombi, hakuomba yoyote, imani yake ilimponya.

54 Sasa marafiki, hii *hapa* Biblia ya Mungu, hiyo ni kweli. Ninayo Biblia ii hii, Biblia hii ambayo nyinyi, walinipa huko Houston, Texas, huko nyuma kabisa katika mwaka wa 1947, nami nilikuwa na Biblia ii hii wakati huo, Mungu aliyeiandika Biblia anajua hiyo ni kweli.

55 Yapata saa tisa usiku, nikasema, "Nitamwombea kila mtu atakayekuja mstarini." Nikasimamisha upambanuzi papo hapo, ili niweze kuwaombea wote. Na kwa hiyo basi, yapata saa tisa usiku, niliwaona wakipita wamelowa maji, huku juu kabisa

*hapa* ndani. Nami nikasema, “Loo,” nikamwambia mkalimani, “mbona, wamelowa maji hivi?”

56 Kasema, “Wanapitia majini, pasipo kungojea kushuka kwenda kwenye kile kivuko yapata maili kumi,” kasema, “walitoka wakaenda jangwani na kuwachukua wapendwa wao, kisha wanavuka mto pamoja nao.” Nao walikuwa wakiwaleta kwa kila kitu.

57 Kwa hiyo, nikaangalia na kulikuwako na askari mkubwa mno, mkakamavu, amesimama pale, na midomo yake samawati kabisa, naye alikuwa akitetemeka. Ndipo nikaangalia, kulikuwa na mzee, yeye na jamaa mwingine walikuwa kwenye u—ubao. Nao walikuwa na u—ubao umewekwa namna *hii* ukiwa na ubao wa msalaba juu yake, na mmoja juu namna *hii*, nao walikuwa wameweka miguu ya huyo mzee juu ya vile—vile vijiti viwili vilivyokingamana namna *hii*, na viwili upande *huu* walikuwa wameiwekelea mikono yake, naye alikuwa akitetemeka kwa kupooza namna *hiyo*, ameota mvi tu alivyoweza kuwa.

Nikamwambia, nikasema, “Unazungumza Kiingereza?”

Akasema, “Kidogo.”

Nikasema, “Unahofu utashikwa na nimonia namna hiyo?”

“La.” Kasema, “Yesu Kristo amenitunza, nilimleta baba yangu.” Imani rahisi!

Nikasema, “Loo.” Nikasema, “Unaamini Mungu atamponya baba yako?”

“Naam, nisingemleta.”

Nikasema, “Mpishe.”

58 Hapana shaka alikuwa ni ndugu yake kule nyuma, alifanana naye sana, basi akapita, akapitia hapo, nikamwekea mikono huyo mzee, nikasema, “Mungu wa Mbinguni, mbariki mzee huyo, mpe shauku ya moyo wake.” Nikampisha.

59 Aliyefuata, nikamwekea huyo mikono. Muda si muda, nikasikia kelele nyingi huko nje, huyu hapa yule mzee amebeba ule ubao begani mwake, akitoka nje, akimpungia mkono kila mtu namna *hiyo*. Loo!

60 Imani rahisi tu, hivyo tu. Hawaninii . . . Wote hawajafungwa kabisa na *hili* na *lile*, wao—wao wanaamini tu, hivyo tu. Sasa, Mungu na atusaidie usiku wa leo, kuwa na imani ya Kihindi, hiyo ni kweli, kuamini.

61 Mungu akimponya huyo msichana mdogo, itakuwa ni ishara, hiyo ni kabla sijaenda San Carlos mara ya kwanza, nikaenda kule, kwa sababu Mungu alimponya mwa—mwanamke aliyekuja kwenye mstari wa maombi, ambaye alikuwa ni mlevi sugu, na aliyefuata alikuwa na kifua kikuu, hao Wahindi wawili. Nao wakarudisha cheti kutoka kwa daktari, kwamba, yapata mwezi mmoja baadaye, nilipokuwa California, ya kwamba

mwanamke huyu aliruhusiwa kutoka kwa daktari, TB yake ilikuwa imekwisha. Naye huyo mlevi sugu hakuwa amewahi kunywa tena.

62 Jambo lingine, mwanamke huyo aliinua mkono wake hapa hivi majuzi usiku, akaokoka. Je, bado uko hapa, dada? Yule mwanamke aliyeinua mkono wake huko nyuma, yule msichana? Vema. Hilo ni sawa. Vema. Hilo ni zuri. Unajisikiaje sasa? Mumeo anaendeleaje? Vema? Unaendelea sawa sasa? Sawa. Mungu akubariki. Makazi yenye furaha kwako.

63 Mumewe aliponywa, pia, mlevi sugu. Um-hum. Na ninii tu, na imekuwa ni jambo tukufu kujua ya kwamba mnamtumainia Bwana Mungu. Hakuna kitu kama hicho. Sasa, kama Mungu atafanya hivyo kwa ajili ya nyumba hiyo, atafanya vivyo hivyo kwa ajili ya nyumba yako, ataondoa maradhi, aondoe kila kitu. Mungu hana upendeleo, Anaomba tu imani rahisi kuiamini. Mungu awabariki.

64 Sasa, tulimwacha Ibrahimu, jana usiku. Je, mnamfurahia Ibrahimu? Wakati mmoja, katika . . . nilikuwa . . . nilihubiri mwaka mzima nyumbani kwenye maskani yangu juu ya Ayubu. Basi nikamfikisha ambapo alikuwa kwenye lundo la majivu, nami nikamweka kwenye hilo lundo la majivu yapata majuma sita. Watu wakawa wazuri sana, mwajua, bali walikuwa wamechoka. Hapo ndipo nilipokuwa nikiandaa upeo wangu papo hapo, Ayubu kwenye lundo la majivu, hapo ndipo Bwana alipomfanyia jambo fulani. Dada mmoja mzuri, hakutaka kuniudhi, bali aliniandikia barua, kasema, "Ndugu Branham, kweli utamwondoa Ayubu kwenye lundo hilo la majivu?"

65 Nafikiri—nafikiri kama nitamfikisha Ibrahimu m—mlimani. Lakini jana usiku, nilikuwa nikikusudia kufikia upeo wake, lakini Roho Mtakatifu akanisimamisha, nami nina furaha sana Yeye alifanya hivyo, maana watu walimjia Kristo, na kutii ni bora kuliko dhabihu.

66 Sasa msingi kidogo. Naye mwanangu aliniambia usiku wa leo, kasema, "Baba, ninii, hao ndio kundi zuri sana la watu tuliowahi kuwa karibu nao." Lakini kasema, "Hakika wanaonyesha ya kwamba wana uvumilivu," akasema, "unawaachilia watoke wamechelewa sana."

Nikasema, "Vema, Billy," nikasema, "ninapata mengi kutoka kwa hayo kadiri wanavyopata." Mnaona? "Si—sina budi kuchajiwa, pia."

67 Ilikuwa tu kama mmoja wa hao ndugu alivyosema hivi majuzi kwenye kiamshakinywa kule, ninaamini ilikuwa ni Ndugu Hobson aliyesema, "Sisi wahudumu tunahitaji, daima tunakabiliwa, mkutano, kwenda hospitalini kukutana na kutokuamini, na jukwaani, kutokuamini, na kila mahali pengine, kutokuamini, hatuna budi kukusanyika pamoja,

mwajua, kwa namna fulani kuketi chini ya mwaloni kidogo mara moja moja."

68 Nilikuwa namwalika mhudumu mzee ahubiri kidogo kanisani mwangu, jina lake lilikuwa John Ryan, amepanda Ghorofani usiku wa leo. Naye a—angehubiri kwa muda kidogo, halafu angekimbia huku na kuunyakua mkono wangu, anisalimie kwa mkono.

Usiku mmoja nikasema, "Ndugu Ryan, kwa nini unafanya hivyo?"

69 Kasema, "Ninachaji tu betri, wewe umeketi hapo nyuma ukiomba, nimehubiri nikaishiwa." Kwa hiyo, inatubidi kuchaji betri mara kwa mara.

70 Kwa hiyo, tunaona ya kwamba Mungu alimwita Ibrahimu. Je, yeye alikuwa m—mtu maalum? La, mtu wa kawaida tu. Naye alikuwa ni jamaa mchanga, tayari kwa utumishi? La, alikuwa ni mtu mwenye umri wa miaka sabini na mitano, kabla Mungu hajamwita. Kwa hiyo, mnaona, Mungu hajali umri, wala uwezo, wala sifa, wala . . . Mungu humwita tu yeyote awezaye kumwita. Na kwa hiyo, basi tunaona ya kwamba Mungu alimwambia ajitenge na jamaa yake na watu wake, na, bali alishindwa kufanya hivyo, wala Mungu kamwe hakumbariki mpaka alipotii yale hasa aliyosema afanye.

71 Sasa, hivi tusingeweza kufananisha hilo na kutoa ujumbe kutoka kwake usiku wa leo, kwa kanisa la Kipentekoste? Mpaka tutakapojisalimisha kikamilifu kwa Mungu, katika kutii Neno Lake lote!

Mungu hatupi Roho Mtakatifu, na kusema, "Vema, nimempata. Hakuna lingine."

72 La, bwana, Yeye alikupa Roho Mtakatifu kwa ajili ya matendo, kwa ajili ya Neno, kwa ajili ya utumishi. Mpaka tutakapotii, tuone njaa mioyoni mwetu! Kuna Wapentekoste wa kutosha wanaoketi papa hapa ndani usiku wa leo kuanzisha uamsho wa Kipentekoste kote nchini humu, ambao ungeninii, bila shaka ungefanya mambo karibu hapa, kama tu tungeufanya moto uwake vizuri, mwajua, na kupata upepo mkali ukivuma kutoka Mbinguni, kama upepo wa nguvu ukienda kasi, jambo fulani lingetukia.

73 Kwa hiyo basi, tulimwacha Ibrahimu, jana usiku, wakati alipokuwa amerejeshwa kuwa kijana. Sitawaulizeni iwapo mnaamini hilo au la, bali mimi—mimi mwenyewe ninaliamini, bali hilo halilifanyi kuwa sahihi. Lakini jambo fulani lilitukia kwa Sara na Ibrahimu. Tunajua hilo, sivyo? Jambo fulani lilitukia, kwa sababu alikuwa tasa, naye mkewe hakuwa na uwezo wa kushika mimba. Nao walikuwa na umri wa miaka mia moja, alikuwa, naye mkewe alikuwa, basi mwanamume angempendaje mwanamke mwenye umri wa miaka mia moja? Kamwe siwezi . . .

Sasa, mtu fulani alisema, “Loo, waliishi muda mrefu zaidi siku hizo.”

74 Ndugu yangu, soma Maandiko hapo, yalisema, “Wote wawili walikuwa na umri mkubwa.” Walikuwa wazee. Nasi tunaona, kwamba si hayo tu, bali nguvu zake zilifanywa upya, naye akawa mwanamke mchanga, mrembo, naye Ibrahimu alikuwa ameurudia ujana, nao walikuwa wakifurahia maisha. Pia kumbukeni, mara baada ya wao kuondoka, kule Gerari, Sara akawa mama na akamzalia Ibrahimu mwana.

75 Hivi hamna furaha sana kwamba tutarudia ujana? Sijui la kusema hapa, ninafurahia hilo sana. Ninajua, nita—nitaahidi kuwaachilia mtoke mapema kidogo, lakini jambo fulani liko moyoni mwangu, sina budi kulisema.

76 Sasa, ninataka kufanya jambo hili dhahiri kabla sijalisema: Ninaamini ya kwamba karama na miito havina majuto. Sasa, Biblia inasema hivyo. Unaona? Si jambo unalofanya, ni jambo ambalo Mungu anafanya. Unaona? Hakuna mtu… U—unasema, “Nilimtafuta Mungu, na kumtafuta Mungu.” La, hukumtafuta, Mungu alikutafuta, na kukutafuta. Haikuwa ni wewe ukimtafuta Mungu, ni Mungu akikutafuta. Unaona? Huo ulikuwa ndio mwanzo, mwanadamu akijaribu kujificha, Mungu akiita. Ndipo Yesu akasema, “Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Mnaona? “Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu.”

77 Sasa, sasa angalieni, tangu nilipokuwa mvulana mdogo wa yapata umri wa miaka miwili—miwili nilianza kuona maono. Ono la kwanza nililopata kuona lilikuwa kichakani, na—naye Malaika wa Bwana alikuwa mle ndani kama upepo, naye akaniambia kwamba ningeishi karibu na mji uitwao New Albany. Nami nilikuwa na umri wa miaka miwili, nikiishi milimani huko Kentucky, nami nimetumia maisha yangu umbali wa maili tatu ama nne kutoka New Albany, Indiana, umbali wa maili mia mbili, mia tatu.

78 Halafu basi, yakaanzia hapo, yakaendelea kote maishani, wala hakuna hata wakati mmoja ambapo yamewahi kukosea, lakini hili, siamini, lilikuwa ni ono. Ninataka kukiri jambo fulani, sikuzote kidogo niliogopa kufa, hata tangu nimekuwa Mkristo. Si kwamba hata nilihofia ningepotea, bali si—sikutaka kuwa ro—roho. Nami daima niliwazia kama tukifa, tungekuwa na mwili wa kiroho, nami ningekutana nanyi watu huko juu, nami ningesema, “Vema, hao ndio watu niliowahubiria huko chini Yakima. Loo, jamani, laiti ningalikuwa na mkono wa kuwapa, bali mkono wangu unaozea kaburini, yao inaoza, pia,” na kwamba hatuna hisi hata kidogo, kama tu wingu dogo, jeupe, mwili wa kiroho, mfano fulani wa mwili, wa kiroho.

79 Nami sipendi kitu chochote cha mizimu, siwezi kukivumilia hicho, si—si—sikipendi hicho hata kidogo. Mimi, ninaweza tu

kuondoka kwenye hicho upesi sana. Kwa hiyo sininii . . . sikuzote niliogopa sana hicho, nikasema, "Natumaini nitaishi kumwona Yesu akija," kwa sababu nilijua ningerudi kutoka huko, na kuwa na mwili uliotukuka. Lakini ni—nilitaka kujua kama nijuavyo sasa, ili niweze kukutana na ndugu yangu na kumpa mkono, na kuwa na wakati mzuri sana. Nikasema, "Kama ninaweza tu kuishi mpaka Yesu atakapokuja nisingekuwa roho, ningebadilishwa tu. Nisingekuwa na wakati huo wa kupitia."

80 Basi sikuzote niliogopa mauti kwa sababu hiyo. Yapata majuma manne yaliyopita, la, samahani, yapata majuma saba yaliyopita, nilikuwa nimekuja kutoka mkutanoni, nami nilikuwa nimelala kitandani mwangu, na nilikuwa nimeamka asubuhi hiyo, basi nikaamka, na kwa namna fulani nikaweka mikono yangu, ambapo mimi hulala namna hiyo, nyuma ya kichwa changu, na kulalia ubao wa miguu, ama, ubao wa kichwa cha kitanda. Ndipo basi, nikasema, "Vema," nikasema, "Mpenzi, umeamka?" nikamwambia mke wangu, naye alikuwa amelala.

81 Nami nikasema, nililala pale kwa dakika chache, kisha nikasema, "Vema, Bill, una umri wa miaka hamsini." Nijuavyo mimi, nilizaliwa Kentucky ambako hawana kumbukumbu ya kuzaliwa. Nanyi je, mnajua alama yangu ya kuzaliwa ni nini, kumbukumbu ya kuzaliwa huko Kentucky? Ni ule mwaka ambao maskini kile kisiki kilipolipuliwa huko juu kilimani, hilo tu ndilo walilojua.

Wao husema, "Mtoto *huyo* alizaliwa lini?"

"Msimu wa kuchuma nyanya."

"Wakati *upi* wa kuchuma nyanya? *Huyu* alizaliwa lini?"

"Wakati wa kukata mahindi."

"Ni wakati *upi* wa kukata mahindi?"

82 Sasa, hiyo—hiyo ilikuwa ndiyo kumbukumbu ya kuzaliwa huko juu kwenye milima ya Kentucky, kwa hiyo sijui nina umri gani, lakini kwa vyovyote vile, mimi—mimi nina kila sehemu ya huo. Kwa hiyo basi, kwa hiyo basi wakati . . . Hivyo ndivyo mama yangu alivyoniambia, nami nafikiri angekuwa karibu sana kuwa sahihi.

83 Na kwa hiyo basi, nikasema, "Una umri wa miaka hamsini, wala hujamfanyia Bwana chochote bado. Afadhali uharakishe, kwa sababu huenda kusiwe na wakati mwingi sana uliosalia." Ndipo nikasema, "Loo, laiti ningaliishi kumwona Yeye akija! Nachukia kuwa roho." Nikasema, "Si—sitaki kwenda huko nje, ambako siwezi kukutana na watu." Nami nikasema, "Na—nampenda Bwana." Ndipo—ndipo papo hapo . . .

84 Jinsi Roho anavyotenda kazi, kama nilivyowaambia hivi majuzi usiku, haya jukwaani ni maono, bali ni maskini maono madogo, mnayasababisha ninyi wenyewe, mnatumia karama ya Mungu aliyoituma duniani, Roho Mtakatifu. Naye

Roho Mtakatifu hufanya kazi kupitia mkondo fulani. Ni wangapi wanaojua hilo? Ni wangapi wanaojua hata wakati mnaponena kwa lugha, ni Roho Mtakatifu akifanya maombezi? Mnaona? Kwenu ninyi mliokirimiwa karama, na safi ili Yeye aweze kunena kupitia kwenu. Vema, basi ameweka Kanisani, mitume, manabii, waalimu, wachungaji, wainjilisti, na kadhalika. Mnaona? Na Yeye hutumia mkondo huo. Jinsi ningeweza kusimama hapa, na kusimulia mpaka asubuhi mambo yaliyotukia!

85 Sasa, na kwa hiyo basi, Kitu fulani kikaanza kuzungumza nami, na kusema, "Endelea tu kukaza mwendo."

Nami nikasema, "Vema, nimekuwa nikikaza mwendo."

Nacho kikasema, "Thawabu iko mwishoni mwa safari. Thawabu iko mwishoni mwa safari."

Nikasema, "Ninaamini ya kwamba ninii..." Nikawaza, "Ngoja, kwani ninazungumza na Nani?"

Nikaangalia pande zote, nikasema, "Meda?" Mke wangu. Nikasema, "Meda, uko macho?"

Akasema, "Huh?"

Nami nikasema, "Sawa."

Na hili likaendelea, nafikiri, kwa saa moja, nikawazia, "Baba, huyo alikuwa ni Wewe? Huyo alikuwa ni Wewe ukisema nami?"

86 Nanyi mmeisikia hiyo hadithi, yule oposamu, na wale samaki wadogo, na mambo ambayo yametukia huko chini, kwa kawaida, maishani, na kadhalika, hivyo ndivyo tu anavyoanza kuzungumza. Kama tu vile mnavyoisikia sauti yangu.

87 Na wakati huyo *mtu* aliponijia, mara ya kwanza aliponitembelea katika umbo la mwanadamu, hakuwa ono, yeye, ninajua ono ni nini, huyo *mtu* alisimama pale na kuzungumza nami. Akasema, akaniambia ametumwa kutoka kwa Mungu, ya kwamba nilipaswa kuwaombea wagonjwa, naye alikuwa awe...Yeye hakuwa ono, alikuwa *mtu*. Si—sijui yeye alikuwa ni nani, alisema tu alikuwa ametumwa kutoka kwa Mungu. Naye alikuwa amesimama karibu kadiri mkono wangu ulivyo papo *hapo*. Nami nikamwangalia, nikazungumza naye, nikazungumza, nikaongea naye, basi Nuru hii ilikuwa imening'inia juu yake, ikashuka juu yake, ikamwinua kwa miguu, naye akatoweka machoni pangu. Na kila kitu alichosema kimetimia kabisa, vivyo hivyo hasa, mnaona, kwa hiyo ni—ninajua ni kweli.

88 Nayo ile Nuru, ulimwengu wa kisayansi umeipiga picha. Kama nikifa usiku wa leo, ushuhuda wangu ni wa kweli. Kanisa linajua jambo hilo kote ulimwenguni. Ulimwengu wa kisayansi unajua, kwa utafiti ambapo waliipiga picha, katika picha na kuiweka pamoja na George J. Lacy, mkuu wa FBI, wa alama za

vidole na hati, za picha, na kadhalika. Naye ameiweka mle ndani kwa yapata juma moja, na kusema, "Ninaapia taarifa kwamba hiyo si saikolojia, Nuru iligusa lenzi. Nuru ilikuwako." Kisha kasema hivi: "Jicho la kimitambo la kamera halitapiga picha saikolojia." Kasema, "Nuru ilikuwako."

89 Gazeti baada ya gazeti limeichukua. Tumekuwa nayo mara kadhaa huko Ujerumani, na Uswisi, na mahali pengine ambapo wameipigia, kisayansi, katika nchi hiyo, imethibitishwa ya kwamba ilikuwa ni ki—*Kitu fulani* cha kimbinguni, kama Nguzo ya Moto ikishuka na kufanya hivyo. Mnaona athari yake humu kanisani. Inatenda kazi kama tu ilivyofanya wakati ilipokuwa duniani katika mwili wa Mwana wa Mungu, sasa iko duniani katika miili ya wana wa Mungu waliofanywa wana wenye mamlaka, ikilikusanya Kanisa pamoja kusudi Mwana wa Mungu aje amchukue Bibi-arusi. Amina. Hiyo ni kweli kabisa.

90 Na sasa, nikiwa nimelala pale, nilimsikia akisema, "Endelea kukaza mwendo. Thawabu iko mwisho." Nami ni—nilihisi nikipatwa na jambo fulani. Nami nikasikia wimbo huo ukiimbwa, tunauimba kanisani mwetu:

> Ningependa kusikia kengele tamu za bandarini zikilia,
> Ingeiangaza imani yangu na ingeondoa hofu zote,
> Bwana, jalia niangalie ng'ambo ya pazia la wakati.

91 Mmeusikia, wengi wenu, ule wimbo mzuri sana wa kale. Nayo ikaninii, nikafikiri kitu fulani kilikuwa...Nilifikiri nilikuwa nikifa, ndipo nikaangalia nyuma, nami huyo hapo nimelala kitandani. Nami nikageuka upande *huu*, na ilikuwa kama ki—kilima kikishuka, moja kwa moja mbele yangu, popote pale.

92 Kumbukeni, huku Biblia yangu ikiwa moyoni mwangu, ninasema kweli. Ingenifaidi nini kusema hivyo kama haikuwa ni kweli? Mahubiri yangu yangefaa nini? Kujitolea kwangu kwote na mateso yangu, nini, ingefaa nini kama mimi ni mwongo? Mnaona, isingefaa kitu hata kidogo. Si lazima niseme jambo hili, bali ninalisema kusudi lipate kuwasaidia, kwa sababu ni kweli.

93 Popote mahali hapo palipo, iwe ni kiwango kingine nisingeweza kuwaambia, lakini nilikuwa mahali fulani ambapo ningeweza kuangalia nyuma. Na kila mtu sikuzote amenishutumu kwamba mimi ni mchukia wanawake. Si—siwachukii wanawake, la, bwana, siwachukii. Na—nawapenda dada zangu, ila sipendi jinsi baadhi ya wanawake hawa wa kisasa wa Marekani wanavyovalia, na kutenda, na kuvuta sigara, na kunywa pombe, na kufanya yasiyofaa, ni aibu kwa taifa.

94 Ndiyo msaliti mkuu kuliko wote tuliyepata kuwa naye, ni vile wanawake hawa wa kisasa wanavyofanya na kadhalika, wakati hata hawawezi kumlea mtoto wao kwenye titi, inawabidi kumpa maziwa ya ng'ombe, atakufa katika miezi kumi na minane kwa sababu ya sumu ya nikotini. Naam, bwana. Ati mnanena juu ya msaliti? Haya basi. Hilo ndilo linalovunja mgongo wa kila taifa, ni uwanawake wake, imekuwa hivyo sikuzote.

95 Nawapenda wanawake halisi, mama halisi. Mungu atupe akina mama halisi wa mtindo wa kale, ili kwamba, tusingekuwa na uhalifu mwingi sana wa watoto kama tungalikuwa na mama aliyekaa nyumbani kuwashughulikia watoto wake, badala ya kwenda nje mahali fulani kwenye karamu za kokteli, na maskini yaya akijaribu kumshughulikia, mahali fulani. Hiyo ni kweli. Hilo ndilo linalotia sumu akili za watoto.

96 Marekani imeozeshwa nao kabisa, inazidi kudhoofika wakati wote, na itaendelea kuwa mbaya zaidi. Hakuna kitu. . . Ninaweza kutoa sauti yangu dhidi yake, bali linaendelea, kwa sababu Maandiko yalisema hivyo. Litakufa katika ujana wake, taifa hili. Sasa kumbukeni, katika Ufunuo 13 wakati lilipotokea, sikuzote lilikuwa la ujana, maskini yule mwana-kondoo aliyetokea.

97 Sasa, kwa hiyo kidogo niliwakemea wanawake, na labda jambo hili limenifanya kuwa chini kidogo tu. Basi ilitokea niliangalia, hawa hapa wakinijia, na kulikuwako, ilionekana kama, wanawake milioni moja. Walikuwa vijana, walionekana kuwa na umri wa yapata miaka ishirini, nao, kila mmoja wao, alikuwa, sasa samahani, akina dada, kwa tamshi hili, lakini wao, kila mmoja, alikuwa mchanga sana, walikuwa na nywele ndefu kufikia kiunoni mwao, wamevaa nguo nyeupe, nao walikuwa miguu mitupu. Nao wangenikimbilia, na kunikumbatia kwa mikono yao, na kupiga mayowe, "Ndugu yangu wa thamani!"

98 Vema sasa, natumaini ya kwamba nimepata neema machoni penu, kwamba mtanielewa, nyinyi humsikiliza daktari wenu, mimi ni ndugu yenu. Sijali, nilipokuwa ninii—nilipokuwa mwenye dhambi, niliishi mwaminifu hivyo, maana Malaika aliyekutana nami, alisema, "Kamwe usivute sigara, kunywa pombe, wala kuuchafua mwili wako kwa njia yoyote," hayo yalikuwa maisha machafu. Mungu Mbinguni anajua ninaishi hayo. Lakini hakuna mwanamume, ambaye—ambaye ana damu nyekundu na mwenye afya ambaye mwanamke angeweza kumkumbatia, simaanishi mtu huyo angekuwa makosani, ama kuwazia mabaya, bali kungekuwako na mhemuko wa kibinadamu, lakini mahali hapo, haukuwepo, ilikuwa ni dada kweli. Nao. . .

99 Ni—niliangalia, nami nikasema. . .Siwezi kuelezea ilikuwa ni nini, hakukuwako na jana, hakuna kesho, ilikuwa ni

*sasa*. Hawakuchoka, hata hivyo wangeweza kupeana mikono, wangeweza kuzungumza, walikuwa na mwili na kama tu walivyokuwa hapa, ila ni vijana tu. Nami nikasema, "Sielewi hili."

Ndipo ile Sauti iliyokuwa juu yangu ikasema, "Hii ni kama, kitu kama Yakobo, wakati alipokuwa amekusanyika pamoja na watu wake."

100 Hapo tu nikaangalia, nao wanaume walikuwa wakija, loo, karibu na kundi hilo, kama tu mamilioni yao. Nao walikuwa wakikimbia, wakinikumbatia kwa mikono yao, na kupiga mayowe, "Ndugu yangu mpendwa!"

101 Ndipo ninii yangu. . .Mnajua nilikuwa nimeoa hapo awali, naye mke wangu akafa wakati. . .huyo ni mamake Billy, na hiyo ndiyo sababu mimi na Billy hatuachani. Mimi. . .Alikufa alipokuwa na umri wa miezi kumi na minane, na maskini dada yake alikuwa na umri wa miezi minane, alikufa pamoja na mama yake, nami nimekuwa baba na mama, wote wawili, kwa Billy. Ndipo nikamwona Hope akija, akipitia kwenye umati, basi nikawazia, "Hakika ataniita mume wake."

102 Basi aliponikaribia, yeye, ningeweza kumwona, ubarikiwe moyo wake, macho meusi, msichana wa Kijerumani, mwajua, na nywele nyeusi, akanikumbatia kwa mikono yake, akasema, "Ndugu yangu mpendwa."

Nikawaza, "Sielewi hili."

Basi kulikuwako na mwanamke mwingine ambaye tu, msichana pale, aliyenikumbatia kwa mikono yake, na kusema, "Ndugu yangu wa thamani."

Naye akamkumbatia mwanamke huyu, akasema, "Liwazie, hatimaye amewasili pamoja nasi!"

Nao watu hawa, wakanichukua na kuniweka juu ya mahali padogo kama *hapa*, wakasema. . .Nikasema, "Mbona hivi?"

Akasema, "Duniani ulikuwa kiongozi." Kisha akasema. . .

Nikasema, "Silielewi."

103 Na papo hapo, Sauti hii ikanena tena, na kusema, "Hapa ndipo unapokusanyika pamoja na watu wako."

Nikasema, "Nitakapokufa, unamaanisha hivi ndivyo nitakavyokuwa?"

"Naam."

Nikasema, "Loo, kwa nini nikaogopa jambo hili? Hili ni zuri sana!"

104 Loo, jamani, ninii tu, *ukamilifu*, hilo halitaufikia, *adhimu*, hilo lisingeufikia, hakuna neno katika lahaja ya Kiingereza lingeifikia. Mungu anajua ya kwamba ninasimulia hili kutoka moyoni mwangu, lilitukia.

105 Nami ningegeuka mara kwa mara, na kuangalia nyuma, nami hapo nimelala kitandani. Haikuwa mbali sana.

106 Sasa, nimesikia, tangu nimekuwa nikilisimulia, kuna mtu anayeitwa Daktari Price ambaye alikuwa na tukio kama hilo, nalo liko kwenye kitabu. Basi kama mtu yeyote ana kitabu hicho, hakika ningetaka kukisoma, maana ninataka kujua jambo fulani kulihusu. Kwa hiyo basi, alikuwa ni mtu aliyewaombea wagonjwa, miaka mingi iliyopita, kabla ya siku zangu.

107 Ndipo basi nikaangalia tena, na halafu ikasema, "Huu ni wakati utakapokusanyika pamoja na watu wako."

Nikasema, "Hawa wote ni Wabranham?"

Akasema, "La, hao ni waongofu wako."

Nikasema, "Waongofu?"

Kasema, "Unamwona mwanamke yule, ambaye ulikuwa tu ukimshangaa, aliyekukumbatia, na kusema, 'Ndugu mpenzi'?"

Nikasema, "Naam."

108 Kasema, "Alikuwa amepita umri wa miaka tisini ulipomwongoza kwa Kristo." Kasema, "Si ajabu anapaza sauti, 'Ndugu yangu mpendwa.'" Kasema, "Hatazeeka tena, hatahuzunika kamwe, atakuwa hivyo milele."

109 Nikawazia, "Loo, laiti ningaliweza kuishi tena, ningelia, ningeomba, ningeshawishi, ninge—ningefanya kila kitu, kama ingenibidi kuwasukumia ndani, ningemfanya kila mtu aje mahali hapo. Loo, jamani, laiti watu wangeweza tu kuelewa ni nini!"

110 Nami nikaendelea hivyo kwa dakika chache, na kwa ghafla (Mtu fulani, niliposimulia hili yapata majuma machache yaliyopita, mtu fulani kwa namna fulani alilipuuza kidogo.), nikaangalia. . . Nami nilikuwa na maskini mbwa mmoja, aliyekuwa akinielimisha, akisaidia kuilisha familia. Nimewinda maisha yangu yote, maskini mbwa huyu angewashika oposamu, kuuni, vicheche, na kadhalika kwa ajili yangu. Nami ningewinda halafu ninge—ningeuza ngozi hizi, kisha ningenunua nguo za shule, na kusaidia kulisha familia ya watoto kumi.

111 Na kwa hiyo, polisi mmoja alimpa sumu tulipohamia katikati ya mji. Loo, nilipolipigapiga kaburi lake, nilisema, "Fritz, kama kuna Mbingu ya mbwa, utakuwa huko. Nami ninamkumbuka maskini farasi wangu, Prince, jinsi nilivyokuwa nikimpanda nikienda mawindoni, kutega mitego yangu na kadhalika, naye alikuwa ameondoka. Basi nilipoangalia, huyu hapa anashuka kilimani, naye huyu hapa Fritz akija. Ninaweza kuona ulimi huo umetokeza, alipanda juu na kuuramba mkono wangu namna hiyo. Huyu hapa akaja maskini Prince, akapiga kelele, akaweka ninii yake. . .

112 Mtu fulani akasema, "Hakuna wanyama Mbinguni."

113 Hayo tu ndiyo unayojua kuhusu Biblia. Wako wapi hao farasi walioshuka, wakamchukua Eliya? Yuko wapi yule farasi ambaye Mwana wa Mungu anakuja amempanda, farasi mweupe wa vita, aliyelowa Damu? Ni lini mbwa mwitu na mwana-kondoo watakula pamoja, na ninii—nao ndama na simba watakula majani pamoja? Hiyo itakuwa wapi, mnaona, kama wao, hawako huko? Hakika, wako. Mungu hapotezi chochote. Bila shaka, watakuwako.

114 Halafu basi, ilitokea tulininii. . .Niliona, naye akaniramba mkononi. Nikasema, "Kama nimeondoka, kama hii ni Paradiso, ambako ninaungojea Utukufu, ninataka kumwona Bwana Yesu."

Nayo Sauti hiyo ikasema, "Lakini huwezi kumwona sasa, Yeye yuko juu zaidi. Siku moja Yeye atarudi."

115 Ndipo basi hawa wahudumu, na hawa watu wote wakiwa wamesimama pande zote, nikaanza kuwatambua basi, baada ya kuona walikuwa waongofu wangu wa watu niliowajua maishani. Walikuwa vijana, sikuwajua wakati huo, mnaona, walikuwa wamebadilika wakawa vijana wanaume na wanawake.

116 "Loo," nikasema, "yule pale ndugu na dada!" Ni—nilikuwa na furaha sana, si—sijapata kuwa na furaha hivyo maishani mwangu. Nami nikasema, "Laiti ningalijua jambo hili hapo kabla!" Ndipo ni—nikaangalia huku na huku, na kusema, "Unataka kusema Yeye atakuja kwangu?"

Kasema, "Atakuja kwako, Naye atakuuliza juu ya Injili unayohubiri, kwa sababu ulizaliwa kiongozi."

Na halafu, nami nikasema, "Vema, je, itambidi Paulo kusimama kwenye hukumu ile ile Mbele Zake?"

"Hakika."

Nikasema, "Basi Paulo akifaulu, mimi nitafaulu, pia, kwa sababu nilihubiri jambo lile lile alilohubiri, bila kupatana juu ya Neno moja."

117 Na hao watu wote wakapaza sauti, "Tunatumainia hilo!" Kasema, "Ndipo tutarudi duniani na kupokea mwili uliotukuzwa, na kuishi pamoja milele katika hali hii."

118 Mnaona, kila kitu katika Biblia kiko katika utatu, mnajua hilo. Nilisema, hivi majuzi wewe uko katika utatu: nafsi, mwili, na roho. Unaishi katika utatu: jikoni, na sebuleni, chumba cha kulala. Huenda ukawa na vyumba vinane ama kumi mbalimbali, lakini, vyumba vya kulala, na *hiki* cha ziada, bali unaishi tu katika vyumba vitatu. Mungu, Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu katika utatu.

119 Nasi tunaona ya kwamba kuja kwa Kristo kuko katika utatu: Yeye alikuja kwanza kumkomboa Bibi-arusi Wake, anakuja tena kumpokea Bibi-arusi Wake, yuaja tena pamoja na Bibi-arusi Wake, kama Mfalme na Malkia, kutawala katika ule Utawala wa Miaka Elfu, mnajua hilo. Kila kitu kiko katika utatu. Nasi

tuko katika utatu: tuna mwili upatikanao na mauti, mwili uliotukuka, ama, ninamaanisha, mwili wa kimbinguni, halafu mwili uliotukuka. Hatua tatu zinaturudisha kwenye ukamilifu wetu tena, kama katika Edeni.

120 Ndipo basi nikasema, "Vema, nimehakikishiwa hilo."

Na papo hapo tu, Sauti ikasema, "Wote uliopata kuwapenda, na wote waliopata kukupenda, Mungu amekupa wewe."

121 Ndipo nikahisi jambo fulani likinipata, nikasema, "Hakika, si lazima nirudi!" Nami nikalihisi limekaribia zaidi kidogo, ndipo nikageuka na kuangalia nyuma kwenye mwili wangu, nami nikajiona nikisogea kitandani, katika dakika chache nilikuwa nimerudi.

122 Ndugu, dada, hilo lilinifanyia jambo fulani. Ninatambua sasa ya kwamba maskani hii iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tunayo moja tayari inayongoja, mwili unaongoja. Nao huo, nafikiri sasa, unaendana na ule Ibrahimu na Sara walikuwa wameupokea, mwili wa namna hiyo, tamshi moja tu ama mawili, halafu nifikie upeo wa ujumbe wangu, ndipo tutaanzisha mstari wa maombi.

123 Mungu alikuwa ameonyesha katika Sara na Ibrahimu hapa, kile hasa atakachowafanyia Uzao wote wa Ibrahimu na Sara. Uzao wote wa Ibrahimu unapaswa kuwa hivyo. Na hapa duniani, Yeye aliwarudisha wakawa kijana mwanamume na kijana mwanamke.

124 Nami nilisimulia hadithi hiyo kwa makini sana nijuavyo jinsi ilivyotukia. Nami, ilikuwa. . . Sininii. . . Msininii. . . Hebu tuliite ono, maana kama ningesema kwamba ilikuwa ni kuhamishwa kidogo pale. . . kama lilikuwa ni ono sikuwahi kuwa na kitu kama hicho. Sasa, sijaribu kumwiga yule Mtakatifu Paulo mashuhuri, maana mimi sininii. . . Ninaona mengi sana ya hayo maishani mwangu, kujilinganisha kimwili. Lakini tuseme ilikuwa ni kuhamishwa kidogo, nilienda kwenye Mbingu ya kwanza, na kama wao, ndivyo ilivyo katika Mbingu ya kwanza, Paulo aliona nini alipoenda kwenye ya tatu? Jamani! Si ajabu yeye alisema, "Jicho halijaona, wala sikio halijasikia." Kama ni tukufu namna hiyo katika Mbingu hii hapa, unapoingia katika Mbingu ya tatu ni kitu gani ambacho huyo ndugu hapana shaka aliona?

125 Sasa, sasa, mara baada ya hayo, baada ya wao kurudi, Mungu aliwafanya upya, aliwafanya kijana mwanamume na mwanamke, alianza upya, wote wawili walikuwa wamerutubishwa wakati huo. Ndipo wakamzaa mvulana mdogo, ambaye aliitwa Isaka. Ibrahimu alimtahiri siku ya nane na akafanya karamu, na, walipomwachisha maziwa, na kadhalika. Halafu basi, tunaona ya kwamba anakua kufikia umri wa kama, hebu tuone, yapata umri wa miaka kumi na miwili, mvulana mdogo tu wa Kiyahudi, mwenye sura

nzuri, aliye na nywele nyeusi, za mawimbiwimbi, na macho madogo, meusi. Na jinsi ambavyo hapana shaka baba na mama walimpenda sana mvulana huyo mdogo!

126 Ndipo usiku mmoja, Bwana akamwamsha Ibrahimu, Naye akasema, "Ibrahimu." Sasa, hebu nikomee tu hapo, Yeye alimwita Ibrahimu, bali nataka kusema jambo hili, hili si Maandiko, bali hakika litaambatana na Maandiko, "Ibrahimu, ninataka kuonyesha Uzao wako tangu sasa, jinsi ambavyo mtu atafanya wakati kweli ananiamini Mimi. Ninajua nilikuahidi mvulana huyu miaka ishirini na mitano iliyopita, wala hukusita kwa kutokuamini ahadi Yangu, bali uliiamini.

127 "Sasa, ninataka kuwafanya watu walioko Yakima, na mahali mbalimbali, ambapo Injili hii itahubiriwa, wajue ya kwamba Mimi hulitimiza Neno Langu. Nitawapa majaribu maradufu ku—kuonyesha ya kwamba watu wanaolikubali Neno Langu, haijalishi kijacho wala kiendacho, hawana budi kulishikilia Neno Langu.

128 "Sasa, ninakupa huyu mwana, sasa nataka umpeleke huyo mwana juu ya mlima fulani ambao nitakwambia. Nitafanya kutoka kwako, kutoka kwa uzao wako hapa, taifa lenye nguvu kutokana na mvulana huyu, nami nitafanya, pia, mataifa yote ya dunia, wewe utakuwa baba wa mataifa mengi. Na sasa, ninataka uchukue tumaini pekee ulilo nalo la Mimi kamwe kuitimiza ahadi Yangu kwako kuwa baba wa mataifa, nataka umpandishe juu mlimani ukamwue. Angamiza kila kitu kinachotoa ushahidi kwamba utaipata."

129 Loo, natumaini mnalipata hilo! Basi bila shaka, maskini mzee Ibrahimu, hakutaka kumwamsha Sara na kumwambia habari zake, kwa hiyo akaamka mapema, akamchukua huyo mvulana mdogo, na wale watumishi wawili, na maskini nyumbu, naye akakata kuni na kuziweka kwenye gunia, ama chochote kile, kisha akaelekea nyikani.

130 Sasa, mtu yeyote wa kawaida. . . Nilipokuwa kwenye doria kwa miaka saba, ilinibidi kutembea kwa wastani maili thelathini na mbili kwa siku kupitia nyikani, nasi tuna miguu ya petroli siku hizi, hao watu iliwabidi kutembea kila mahali walipoenda. Mtu wa kawaida, anapaswa, tuseme, anapaswa kutembea maili ishirini na tano kwa siku. . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

131 . . . angalia vitu usivyoviona kwa jicho lako. Huoni kwa jicho lako kwa vyovyote vile, unaona kwa moyo wako, unaangalia kwa jicho lako. Kwa hiyo, mkisimama kwenye mlango huo wa imani. . . Angalieni aliyosema Yesu, hapa, hebu nisome hapa, "Kwa kuwa unasema mimi ni tajiri, tena nimejitajirisha," angalieni makanisa yetu, tulikuwa huko chini kichochoroni, tulikuwa pembeni tukiwa na tari, lakini sasa tuna baadhi ya majengo yaliyo bora sana nchini, wakati mwingine, baadhi ya

wasomi hodari sana mimbarani, "kwa kuwa wasema ya kwamba mimi ni tajiri, tena nimejitajirisha, wala sina haja ya chochote; nawe hujui ya kuwa wewe ni maskini, mnyonge, uchi, kipofu, nawe hujui."

132 Sasa, kama ningemwona mtu mtaani aliyekuwa maskini, naye hata hakuwa na nguo zozote, tena alikuwa kipofu, na kama ningeweza kumwendea na kuzungumza naye kuhusu jambo hilo, na kusema, "Bwana, unatambua kwamba uko uchi?"

"Loo, ndivyo nilivyo, bwana?"

"Naam, ingia humu ndani, nitakupa nguo kadhaa."

133 Lakini vipi kama mtu huyo ni uchi, mwenye mashaka, maskini, na kipofu, naye hajui? Huyo ni mtu asiyewajibika, huo ni upungufu wa akili. Nalo kanisa limepungukiwa kiroho. Hawatambui ya kwamba Mungu anatikisa kila karama mbele ya kanisa, nao hawatambui; vipofu, wala huwajui. Wazia hilo, uchi, mtu aliye uchi, kipofu, maskini, na mwenye mashaka, na mnyonge, naye hajui, hilo linasikitisha. Naye Yesu alisema kanisa lingekuwa hivyo katika wakati huu wa Laodikia, nalo hili hapa.

134 "Mimi ni *fulani-wa-fulani*, mimi ni mfuasi wa dhehebu *hili*, mimi ni mzuri tu kama ulivyo wewe."

135 Lakini, ndugu, Yeye alisema, "Niombe ushauri, ukanunue vazi jeupe." Vazi jeupe katika Biblia linaitwa haki ya watakatifu. "Nunua Kwangu vazi jeupe, ununue Kwangu Dhahabu iliyosafishwa kwa moto," ule moto wa Kalvari. "Nunua Kwangu Dhahabu," Mafuta matakatifu ya Mungu yaliyomwagwa, kununua Dhahabu ya namna hiyo, nunua haki ya watakatifu, upate kufichwa.

136 Na sasa angalieni, "Na ununue Kwangu Dawa kidogo ya macho kwa ajili ya macho yako." Loo, jamani! "Nunua Dawa kidogo kutoka Kwangu ambayo itayafungua macho yako," kwa yale yanayoendelea karibu nasi. Ee Mungu, laiti ningalikuwa na njia fulani ambayo ningeweza kulifanya Kanisa lione hilo. Nunua Dawa! Dawa ni mafuta magumu; nayo Mafuta ni Roho Mtakatifu. "Hebu niyapake macho yako mafuta upate kuona ya kwamba Mimi ni yeye yule jana, leo, na hata milele, nikujalie kuona ya kwamba ahadi nilizotoa kwa ajili ya siku za mwisho, zimewadia. Nunua Kwangu Dawa."

137 Tulikuwa watoto, waliolelewa maskini sana, babu yangu alikuwa mwindaji, mwindaji hodari, aliyejulikana kote nchini kwa kuwinda. Basi hali ya hewa ilipokuwa mbaya, alikuwa akitega, na alipotega alikuwa akitega wanyama wenye manyoya. Naye alikuwa na mbwa, naye akawashika kuuni, rakuuni, nadhani mnao hapa Washington, rakuuni. Naye alikuwa akiwachukua kuuni hao, nasi tungekula hizo nyama, tuuze ngozi, hatukupoteza chochote.

138 Na mafuta yalikuwa tiba-ya kila kitu nyumbani kwetu. Ungekuwa na kikombe kilichojaa mafuta ya kuuni, kama mmoja wa hao watoto angeshikwa na ugonjwa, alidondoshewa matone kadhaa ya terafini juu yake kwa ajili ya mafua makali, na kuyameza. Sijui jinsi tulivyoishi, bali tuliishi. Lakini yalikuwa ni tiba ya kila kitu, kama mtu alipata jeraha, wangelitia mafuta ya kuuni, kuumwa na kichwa, wangekupaka mafuta ya kuuni kichwani mwako.

139 Na ilitubidi kulala ghorofani, ilikuwa ni nyumba ndogo, yenye vyumba viwili ambayo mama, na baba, na sisi watoto watano, kabla ya hao wengine kuja. Tulilala ghorofani, wavulana. Baba na mama, hapakuwako na sakafu ndani yake hata kidogo, sakafu ya udongo, tulitumia kisiki kilichokatwa kama meza, na ndipo wao, chumbani mle, walikuwa na ki— kitanda kilichojengwa kwa. . . kimetandikiwa godoro la nyasi kavu, pamoja na mto wa makapi. Baba alikuwa na brashi ya kunyolea iliyotengenezwa kwa makapi. Tulikuwa huko juu sana milimani.

140 Nyanya yangu alikufa akiwa na umri wa miaka mia moja na kumi, na kamwe hakuona garimoshi maishani mwake, aliona tu gari moja, nami nililileta kule juu, na ilinichukua siku nzima kusafiri maili nne, nikijaza mawe kijitoni ili niweze kulipandisha huko juu, majirani wote wakisimama huko nje, hawakuwahi kuona kitu kama hicho maishani mwao. nilipoipandisha Chevrolet hii ndogo ya '26 kupitia milima hiyo, Nikakwamia kule chini, nami nikamwomba huyo mtu kama angemchukua farasi wake, alikuwa akilima, kasema, "Farasi jike wangu, ukimleta karibu na pale, angekirarua kitu hicho vipande-vipande, kamwe hakuwa amewahi kuona kitu kama hicho."

141 Kwa hiyo, tulikuwa maskini. Halafu tulikuwa tumekata miti michache, nayo ilikuwa na orofa ya juu wakati familia kidogo ilipokuwa kubwa, dari, nyufa kubwakubwa kwenye magogo, ambamo mianya, udongo ulikuwa umeporomoka, maskini viezekeo vya mbao vilichomekwa kuziba mwangaza wa mwezi, vimepinduliwa. Tulilala mle usiku. . . Naye Mama angetufunika kwa godoro la manyoya msimu wa baridi kali, kisha angeweka makoti yote yaliyochakaa, na vitu tulivyokuwa navyo, halafu kipande cha turubai, mahali iliponyeshea, tungejipenyeza tu chini ya turubai hilo kama sungura, kama mvua ilinyesha ama theluji kuanguka. Nawe ungeweza kulala mle na kuhesabu nyota wakati wowote.

142 Ndipo kikaja kipindi cha baridi, na kama hatukuingia chini ya turubai hilo, macho yetu yangeshikwa na baridi. Na kungekuwa na. . . Mama aliyaita *matongo*, sijui ni nini, lakini yangeyafunga macho yetu. Nami ingenibidi kuamka asubuhi, kuwasha moto, nishuke kwenye miti hii michanga

iliyokingamishwa kwa vijiti, kisha niwashe moto katika jiko kubwa kuukuu.

143 Na kwa hiyo basi, Mama angeniita asubuhi, naye angesema, "Billy!" Ubarikiwe maskini moyo wake.

Ningesema, "Naam, Mama?"

Angesema, "Shuka uje, ni saa kumi. Baba yako hana budi kuondoka."

144 Nami ningejaribu kuamka, mimi na ndugu yangu, nayo macho yetu yangekuwa yamejaa matongo, yote yamefungamana, baridi imesababisha hilo. Ningesema, "Mama, siwezi kuona."

"Mwite Edward, ndugu yako."

Ningesema, "Hawezi kuona pia, Mama, macho yake yamejifunga."

145 Mama angeenda kwenye jiko dogo bapa jikoni, lililowekwa juu ya vipande vidogo, naye angewasha moto, na kwenda na kuchukua kopo la mafuta ya kuuni, aliweke juu ya jiko na kuyapasha moto. Angepanda kule juu na kuyasugua macho yetu kwa mafuta hayo ya kuuni. Yalifanya kazi vizuri, tuliweza kuona baada ya yeye kuyasugua macho yetu kwa mafuta ya kuuni.

146 Ndugu, tumekuwa na upepo mwingi sana wa kiroho, ubaridi mwingi umelipiga kanisa, itahitaji zaidi ya mafuta ya kuuni kuyafungua macho yetu, itahitaji Roho Mtakatifu wa Mungu, Dawa Yake ya macho kuyafungua macho. Tumekuwa na theolojia nyingi sana, "Siku za miujiza zimepita. Hakuna kitu kama uponyaji wa Kiungu, ni telepathia tu ya kiakili. Usisikilize chochote juu yake. Msiwakaribishe mjini mwenu. Wao ni *hili*, *lile*, *linginelo*." Itahitaji zaidi ya mafuta ya kuuni kuyafumbua macho yetu, ambayo yamepigwa na upepo wa namna hiyo.

147 Lakini Mungu ana Mafuta yatakayofanya hivyo, naam, bwana, yatafanya hivyo. Ndipo utakapoyafungua macho yako, utakuwa kama Gehazi alivyokuwa pamoja na Elisha huko Dothani. Mnakumbuka usiku ule yule nabii wa kale aliposhuka akaenda kule na kulala? Ndipo jeshi la Shamu likaja na kuuzingira mji wote. Naye Gehazi, mtumishi wake, akaamka, akaangalia nje na kulikuwa na kote mjini tu hakukuwako na kitu ila askari, silaha. Na hapo alilala yule nabii mzee mwenye upara, nabii mwenye masharubu marefu amelala pale usingizi, akamtikisa na kusema, "Baba yangu, baba yangu, amka upesi! Tumezingirwa, tumenaswa!"

148 Ninaweza kumwona maskini yule nabii akisimama, macho yake yalikuwa yamefunguliwa, akaamka na kuangalia pande zote, "Naam, ninawaona, lakini kunao wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao." Kuna wengi walio pamoja nasi kuliko wakosoaji.

Akaangalia kote, naye Gehazi angali alikuwa, alihitaji kuchuliwa macho yake, kasema, "Sioni kitu ila Washami."

149 Maskini huyo nabii akanyosha mkono wake, akamwekea mikono, na ishara hizi zitafuatana na hao waaminio, mwajua, ndipo macho yake yakafunguka, akasema, "Bwana, macho ya mtu huyu na yafumbuliwe, apate kuona."

150 Ndipo Mungu akayafumbua macho yake, na kote kumzunguka nabii huyo mzee, kote milimani kulikuwako na magari ya Moto, na Malaika wa Moto; macho yake yalifunguliwa.

151 Laiti tungeyafungua macho yetu kuona alasiri ya leo, Malaika wa Mungu, Roho Mtakatifu, wameketi huku, wamesimama, wakitembea huku na huku kwenye marefu ya kanisa, haleluya, wakizunguka kwenye kusanyiko, ungeona kuna wengi walio pamoja nasi kuliko walio pamoja nao.

152 Mungu fungua macho yetu, fungua mioyo yetu, fungua kila mlango mioyoni mwetu. Kasema, "Nasimama na kubisha, kama mtu yeyote ataisikia Sauti Yangu, na kufungua, nitaingia, na kula pamoja naye."

153 Hebu turudi nyuma kidogo, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, tutafunga, hebu na tujiweke kwenye chumba kidogo kwenye barabara Nyofu inayoongoza, iliyoongoza kuelekea Golgotha. Nami ninamsikia Mtu fulani akija, kunasikika kama kubisha mlangoni, *kung*, *kung*, *kung*, kana kwamba mtu fulani anabisha mlangoni. Tunaenda mlangoni na kufungua mlango. Hakuna mtu mlangoni hasa, bali hata hivyo ni kubisha, bali ni msalaba wa kale unaoparuza ukishuka kwenye mawe ya barabarani, ukikokota alama za miguu zilizolowa damu za Mbebaji, *kung*, *kung*, *kung*.

154 Loo, unapaswa kushuka chini sana leo, nawe unapaswa kuuhisi. Begani Mwake ulikuwa ukisugua, *kung*, *kung*. Inaonekana kana kwamba mtu yeyote angemfungulia huyo mlango, Mtu anayekufa ambaye hakujua dhambi, hata hivyo akafanywa dhambi kwa ajili yetu, kufanya njia ya kugongagonga huko. Ee Mungu, jalia kishindo hicho kifungue kila moyo humu ndani, alasiri ya leo. *Kung*, *kung*, unapoendelea, mwangalie.

155 Wananiambia Yeye hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake. Kasema, "Mbweha wana matundu," maumbile Yake, "ndege Wake wana viota, bali Yeye, Muumba wa Mbingu na nchi, hakuwa na mahali pa kulaza kichwa Chake, wala rafiki wa kusimama karibu Naye."

156 Hivi huwezi kuhisi huko kubishwa kwa mlango alasiri ya leo? [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Alikuwa akifanya hivyo ili kwamba kishindo hicho kipige mlango wa moyo wako ufunguke alasiri ya leo, kumruhusu aingie kama Mungu, na kama Mwokozi, kama Mponyaji, kama Mfalme.

157 Alikuwa na joho moja. Alikuwa amevikwa nguo za kitoto alipozaliwa, hayo ni matandiko kutoka nyuma ya nira ya maksai, hawakuwa na nguo za kumvisha Yeye. Na sasa Yeye yuafa akiwa na vazi moja kwa Jina Lake, hata hivyo Yeye aliumba kila vazi, akaumba Mbingu na nchi. Halina mshono ndani yake, walilitupa mabegani Mwake. Ninaona kuna madoa madogo mekundu juu yake. Ninapoona huko kugongagonga kukififia, je, nitakuacha kupite bila mimi kukukubali?

158 Ee Mungu, jalia mkutano usifungwe mpaka umekukubali, ujue ya kwamba Yeye anagongagonga moyoni mwako. Alikufa ili aweze kurudi hapa katika mfano wa Roho Mtakatifu na kufanya mambo ambayo amekuwa akikufanyia. Fungua moyo wako, mwamini Yeye.

159 Ninaona anapoenda juu ya hayo madoa madogo mekundu, yanazidi kuwa makubwa zaidi na zaidi, mpaka yote yanakuwa bonge moja kuu.

160 Shetani alikuwa akitembea pale, akasema, "Haiwezekani kuwa ni Yeye! Huyo hawezi kuwa ni Mungu. Nilimhoji siku moja nikasema, 'Ikiwa Wewe ndiwe Mwana wa Mungu fanya mwujiza na hebu nikuone ukiufanya.'"

161 Ibilisi huyo angali anajibu swali hilo, ama, analiuliza. "Ikiwa una nguvu za uponyaji, hebu nikuone ukimponya *huyu*."

162 Yesu akasema, "Imeandikwa!"

163 "Ndipo basi nikampeleka karibu na askari," Shetani akasema, "nikawafanya askari wangu wa Kirumi walewe nusu, nikamfunga kitambaa kichwani mwake, nikayafunika macho yake, maana, unajua, alisema angeweza kujua mawazo yao, haingembidi kufungua macho yake wakati huo. Nami nikamfunga kitambaa kichwani mwake, nikawafanya askari wangu wamfunge, kisha nikachukua, nikawafanya wachukue fimbo na kumtwanga kichwani, kasema, 'Tuambie ni nani aliyekupiga, ikiwa wewe ni nabii.' Alikuwa ni wa bandia, asingeweza kutuambia.

164 "Na halafu, nikawafanya hao askari walevi kumtemea mate usoni. Na je, huyo angeweza kuwa ni Mungu katika mwili huo, akienda kule huku mafundo ya mate yakining'inia usoni mwake, taji ya dhihaka kichwani mwake? Nami nikamhoji, na kumpa changamoto afanye jambo fulani, naye kamwe hakufungua kinywa chake, huyo hawezi kuwa ni Mungu."

165 Kwa hiyo walipomtundika msalabani, yeye alisema, "Vema mauti, njoo huku, mchukue, yeye si Mungu." Ninamwona huyo nyuki wa mauti akija huku akivuma kote. Akasema, "La, huyo si Mungu, Mungu asingeweza kupiga mayowe msalabani apate rehema, Mungu asingefanya hivyo."

166 Kuhani mkuu akasema, "Aliwaokoa wengine, lakini mwenyewe, hawezi kujiokoa."

167 Sifa kubwa kuliko zote waliyopata kumpa. Kama angejiokoa Mwenyewe asingeweza kuwaokoa wengine. Lakini alijitoa Mwenyewe ili niweze kuokolewa, na kwamba wewe uweze kuokolewa.

168 Baada ya kitambo kidogo, nyuki huyo alishuka na mwiba wake na kumchoma. Mtu yeyote anajua ya kwamba nyuki, ama mdudu yeyote aliye na mwiba, wakati mara anapochoma ndani sana, hawezi kuchoma tena, kwa sababu mwiba wake hung'oka. Mauti yaliingiza mwiba wake katika mwili mwingine wakati huo, Yeye akaung'oa huo mwiba. Sasa mauti yanaweza kupiga kelele inayovuma, bali ha—hayawezi kuuma tena.

169 Mmoja wao aliyefungua mlango, alisema, "Mauti u wapi uchungu wako? Kaburi u wapi ushindi wako? Lakini Mungu na ashukuriwe, atupaye ushindi kwa Bwana wetu Yesu Kristo."

170 Mauti yanaweza kuvuma na kutenda kana kwamba yatauma, bali hayawezi kuuma moyo ambamo milango yote imefunguliwa, naye Mwana wa Mungu anaishi na kutawala moyoni. Hivi humtaki katika wako alasiri ya leo, wakati kugongagonga kwa msalaba kunaendelea? Huyo ni Yeye amesimama, akisema, "Ninasimama mlangoni, katika wakati wa Laodikia na kubisha, na kama mtu yeyote ataisikia Sauti Yangu, na kufungua, nitaingia na kula."

171 Je, utakula pamoja Naye? Je, utamfanya Bwana? Je, utamruhusu ayatawale maisha yako? Je, utamruhusu akuongoze na kukuelekeza? Kama ni kinyume na mawazo yako, wewe—wewe yaachilie mawazo yako, "Nia ya Kristo na iwe ndani yenu." Je, utafanya hivyo, tunapoinamisha vichwa vyetu kwa muda kidogo tu kwa ajili ya maombi?

172 "Ninasimama na kubisha." Angalia kile alichokufanyia, kugongagonga kwa msalaba. "Mtu yeyote akiisikia Sauti Yangu, na kufungua, nitaingia. Ndipo aniketishe chini, na kunipa kiti, na kunifanya nijisikie nimestarehe, si huzuni. Sio kumwacha aseme, 'Sikutaki katika maisha yangu ya kibinafsi, nina imani ya kutosha, sikuhitaji tena kwa ajili ya jambo hilo.' Usifanye hivyo, bali nikaribishe, nipe kiti, kiti kizuri, cha starehe, na kusema, 'Naam, Bwana. Hii hapa sifa kidogo moyoni mwangu. Huu hapa mkono wangu ukiinuliwa, mlo mdogo tu. Huu hapa mchuzi kidogo ambao tungeweza kunywa pamoja, tuketi na kuongea pamoja Nawe.'"

173 Je, ungependa kufanya hivyo? Inua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, sasa nataka, Yeye ale pamoja nami, ninataka kula pamoja Naye." Mungu akubariki, mama. Wengine, kunaweza kuwako na mwingine? Mungu akubariki, mama. Mungu akubariki, bwana. Mungu akubariki, ewe kijana. Mungu akubariki, dada. Vema.

174 Mtu mwingine kwenye orofa ya chini, kabla hatujaenda kwenye roshani, inua mkono wako, useme, "Bwana ingia, ni—

ni—ninataka ule pamoja nami, ninataka uzungumze nami. Na—nataka kukufanya Bwana moyoni mwangu. Nilikuhisi ukibisha, na—nataka ule pamoja nami." Inua mkono wako, mtu mwingine ambaye hajainua mkono wake kwenye orofa ya chini, angehisi msukumo huo sasa hivi. Je, unaweza kuhisi mgongano wa msalaba huo? Mbona, linapaswa kufanya kila msuli ndani yako utetemeke kujua ya kwamba Yeye alikufanyia hilo! Nawe hutaweza angalau kumwinulia mkono wako? Si angalau kuinua huo mkono! Mungu akubariki, huko nyuma, bwana.

175 Juu kwenye roshani mkono wangu wa kushoto, naomba uinue mkono wako. Ninyi mlioinamisha vichwa vyenu, semeni, "Kula pamoja nami, Bwana." Mungu akubariki hapa, ndugu yangu mweusi. Mungu akubariki, mvulana mdogo, uliyeketi hapo. Mtu mwingine huko juu kwenye roshani?

Useme, "Hilo litafanya lolote, Ndugu Branham?"

176 Kama kweli unalimaanisha, umepita kutoka mautini kuingia Uzimani, Ataingia ndani moja kwa moja. Umeuhisi msalaba moyoni mwako alasiri ya leo, hayo matuta chini mtaani, Yeye akijaribu kubisha mlangoni pako apate kuingia kukufanyia jambo jema? [Ndugu Branham aligongagonga mimbarani—Mh.] Inua mkono wako.

177 Roshani mkono wangu wa kulia, kwenye kusanyiko hilo hapo, tafadhali inua mkono wako, useme, "Ndugu Branham, niombee. Mimi sasa . . . " Mungu akubariki. Mungu akubariki. Hilo ni zuri. Mtu fulani . . . Mungu akubariki. Ubarikiwe. Mbariki yule mtoto pale. Mbariki huyu. Hiyo ni kweli. Mtu mwingine, inua tu mkono wako. Mungu akubariki. Mtu mwingine? Aisee, kama . . . Mungu akubariki, hapa nyuma, bwana.

178 Mtu mwingine? Naam, mvulana mdogo aliyeketi hapa. Loo, wakati mwingine hiyo mioyo midogo ambayo haijakokotwa kupitia kwenye mambo mengi ya kusikitisha na mambo ya ulimwengu, ni laini. Mnajua, Biblia ilisema katika Isaya 10, "M—mtoto atawaongoza."

179 Hivi hutainua mkono wako, kabla tu hatujasimama sasa? Mungu ambariki huyo msichana mdogo. Mungu ambariki jamaa huyo mdogo hapo. Mtu mwingine? Inua mkono wako. Useme, "Sasa nataka . . . Ninahisi tuta." Mungu akubariki, ewe msichana, Mungu awe pamoja nawe, hilo ni jambo la kishujaa kufanya, Mungu daima awe pamoja nawe. Usiogope, ndilo jambo kuu sana ulilopata kufanya, mpenzi. Siku moja mauti yatakapokuja, utakumbuka ya kwamba ulifanya jambo sahihi, utakumbuka jambo hilo kabla ya wakati *huo* kutokea. Ubarikiwe maskini moyo wako.

180 Mtu mwingine? Inua mkono wako, useme, "Ninahisi kugongwa na kubishwa mlangoni pangu, Ndugu Branham, nitafungua mlango wangu na kumwangalia, ndipo nitakapoiona

ile Damu pale, na kujua ya kwamba ni Yeye, nitasema, 'Karibu, Bwana. Ingia ndani, uketi chini, chukua kilicho bora kuliko vyote nyumbani mwangu, nitakukaribisha. Nitaenda kumwambia kila mtu kwamba Yesu aliingia maskini makazi yangu alasiri ya leo, maskini moyo wangu mdogo. Sio sana, lakini hakika Yeye aliujia na kubisha mlangoni, nami nikamruhusu aingie, Mtu muhimu sana ambaye angeweza kubisha mlangoni pangu." Usimkatae.

181 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, tunapofanya wito wa madhabahuni, kwa uchaji, kwa utulivu. Nitaliacha tu ligonge kwa dakika chache. [Dada mmoja ananena kwa lugha, dada mwingine anafasiri—Mh.]

> Usinipite, Ee mpole . . .

Je, utasimama kutoka kwenye kiti chako, ukija kwa maombi sasa?

> . . . kilio changu kinyenyekevu;
> Unapozuru wengine,
> Usinipite.
>
> Mwokozi, . . .

182 Utakuja sasa na kusimama madhabahuni?

> Kisikie kilio changu kinyenyekevu;
> Unapozuru wengine,
> Usinipite.

183 Kwa nini usisimame sasa na uje madhabahuni hapa? Wewe unayetaka kuufungua mlango huo wa moyo, umwache Yeye awe Bwana maishani mwako, njoo usimame hapa kwa ajili ya maombi kabla tu hatujaanzisha mstari wa maombi. Hivi hutakuja?

184 Tungefurahi kuwa pamoja nanyi hapa, wachungaji watawakaribisha moja kwa moja ndani. Haiwabidi kwenda mahali pengine popote, wana makanisa papa hapa, mengi yao yanayoamini Injili ii hii, nao bila shaka watashughulikia ninii, ninyi. Mungu akubariki, mama, hiyo ndiyo njia sahihi ya kufanya hilo.

185 Tunapoimba tena, mtakuja sasa? Hebu kila mtu aliyeinua mkono wake aende na kusimama madhabahuni kwa ajili ya maombi, sivyo?

> Usinipite, . . .

186 Simama uje, sivyo? Unakuja kutoka kwenye roshani, tutangojea.

> . . . kilio changu kinyenyekevu;
> Unapozuru wengine,
> Loo, usinipite.
>
> Mwokozi, Mwokozi,
> Kisikie kilio changu kinyenyekevu;

Unapozuru wengine,
Loo, usinipite.

Mwokozi, . . .

Mungu awabariki, kijana mwanamume na kijana mwanamke, Mungu awabariki. Mungu awabariki, ndugu na dada yangu.

. . . changu . . .

187 Hivi hutasimama kutoka kwenye kiti chako, na ushuke moja kwa moja? Hebu wafanyakazi wa kibinafsi waje wakati huu, pia.

Unapozuru wengine,
Usinipite.

188 Nilimwona mmoja wa wavulana wetu weusi wa thamani, nadhani mke wake alikuja akitembea. Mnajua yale ninayowazia hapana shaka yalimjia moyoni mwake? Kulikuwa na mtu mweusi wakati wa tukio hilo, aliposikia huo mgongo, alimtazama akiyumbayumba, Simoni Mkirene, akaenda kule, akaweka msalaba mgongoni mwake, na kusema, "Bwana, ni—nitakusaidia kuubeba kupanda kilimani."

189 Hao hapo wawili wa watoto wake alasiri ya leo, walisikia mgongo huo. Katika saa ya ukosoaji juu ya Kanisa, wako tayari kuubeba msalaba, na kusema, "Bwana, nitakusaidia kuubeba. Haidhuru mtu mwingine yeyote anasema nini, ninakuja moja kwa moja kukusaidia kuubeba." Anakumbuka hilo, Yeye hasahau chochote.

Mwokozi, Mwokozi,
Sikia . . .

Hivi hutakuja? Mtu mwingine?

. . . kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usinipite.

Wewe uliye Kijito cha faraja yangu yote,
U zaidi ya maisha kwangu,
Nina nani duniani ila wewe?
Nani Mbinguni ila Wewe?

Njoo sasa.

Mwokozi, . . .

Njoo uchukue mahali pako sasa.

. . . Ee Mwokozi,
Kisikie kilio changu kinyenyekevu;
Wakati . . .
Usinipite . . .

190 Na tuinamishe vichwa vyetu sasa. Endelea, kwenye kinanda. Huku muziki huo mtamu na mzuri ukipigwa, kwenu mnaosimama hapa, mvulana mdogo, mwanamume mzee, na

mwanamke, mwanamume mzungu, na msichana, mwanaume mweusi na mkewe, kiwete hata anasimama, Ee Mungu, twende wapi mauti yanapotupiga? Hakuna mtu ila Yeye. Wewe njoo, kwa sababu kitu fulani hicho, ulihisi mgongo huo moyoni mwako. Sasa Yeye yuko tayari kukuingiza ndani sasa.

191 Baba yetu wa Mbinguni, imeandikwa, ninalinukuu Neno Lako, nikilinukuu vizuri nijuavyo, katika Yohana Mtakatifu 5:24, haya ndiyo Maneno uliyosema, kulingana na Maandiko: "Yeye alisikiaye Neno Langu," ambalo ndio kwanza walisikie walipokuwa wakibisha mlangoni, "na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele, wala hataingia hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani."

192 Ulisema jambo hilo, Bwana, ninaliamini. Hapo ndipo nafsi yangu imetulia, papo hapo. Uliliahidi, kila ahadi ni ya kweli. Kasema, "Hakuna mtu awezaye kuja Kwangu, asipovutwa na Baba Yangu." Basi nguvu za sumaku za Mungu aliye hai zinavuta alasiri ya leo. "Na yule atakayekuja Kwangu, sitamtupa nje kamwe."

193 Kwa nini? Kwa sababu Baba amezitoa. Walisikia, Mungu akawavuta, nao hawa hapa, isingewezekana kwao kutupwa nje. Ulisema, "Nitampa Uzima wa Milele, na kumfufua katika siku ya mwisho." Hiyo ni ahadi Yako, Baba.

194 Wanasimama hapa mbele ya kusanyiko hili la watu mia kadhaa, nao wanakiri kwamba Mungu alinena nao. Wewe ulisema, "Yeye atakayenishuhudia Mimi mbele za Wanadamu, huyo nitamshuhudia mbele za Baba Yangu, na Malaika watakatifu," basi Wewe unaandika jina lao kwenye Kitabu cha Uzima, Bwana, nakushukuru kwa ajili ya jambo hili.

195 Mara waliposimama kwa miguu yao, Wewe ulikubali utambulisho wao, kwa kuwa wameutupa Kwako alasiri ya leo, Bwana. Walikuwa wenye dhambi, nao wanalia wapate rehema, Wewe wapokee, ulisema utafanya hivyo, hilo linalifanya kuwa hivyo. Waliokolewa mara waliposimama. Wamesimama hapa mbele ya kusanyiko huku vichwa vimeinamishwa sasa, kukuchukua Wewe kama Mwokozi wao, kushuhudia mbele ya kusanyiko hili kwamba wameokoka.

196 Baba, usiache hiki kiwe kikomo, bali jalia wampokee Roho Mtakatifu. Saa imekaribia, hawana haja ya kufanya jambo lingine lolote, bali waingie kazini. Wape nyenzo, chochote kilicho mkononi mwao, wengine wanaweza wakaimba, wengine wanaweza wakahubiri, wengine wanaweza wakashuhudia, hatujui, bali chochote kilicho mkononi mwao.

197 Samsoni alikuwa tu na mfupa wa taya la nyumbu, bali aliwaua Wafilisti elfu moja. Shamgari alikuwa na konzo la ng'ombe, Wafilisti walikuwa wanakuja, hakuwa na wakati wa kujifunza kujua jinsi ya kupiga vita, Roho wa Mungu akamshukia, akachukua konzo la ng'ombe lililokuwa mkononi

mwake na kuwabwaga chini mamia ya Wafilisti. Daudi alikuwa na kombeo, Goliathi alikuwa amempa changamoto, lakini Mungu alikuwa pamoja na hilo kombeo.

198 Nao hawa hapa wamesimama alasiri ya leo, Bwana, kama viumbe vipya, jalia wampokee Roho Mtakatifu. Kama hawana elimu, mafunzo, wala chochote kile, wapeleke kwenye huduma ya utumishi, Bwana, kwa ajili ya utukufu Wako, wakati wamekukubali huko kubisha kwenye mlango.

199 Basi huku mmesimama, na ninyi mliokuja madhabahuni, hata kwa hawa wavulana wadogo, na wote, kama unaamini Yesu Kristo ni Mwana wa Mungu, na kuamini ya kwamba alikufa apate kukuokoa, nawe unamkubali kama Mwokozi wako, inua mkono wako mbele ya kusanyiko hili, wapate kuona ya kwamba unamkubali Yesu kama Mwokozi wako. Kwenu mlio madhabahuni hapa, ndio ninaowazungumzia. Jambo ndilo hilo. Inueni mikono yenu. Hiyo ndiyo njia. Mungu awabariki. Mungu awabariki.

200 Sasa kwa ajili ya baraka za ziada kidogo, kufundishwa, mhudumu amesimama hapa tayari kuongoza chumbani, ambapo tunaweza kukutana nanyi chumbani kwa ajili ya maombi. Sogeeni tu moja kwa moja upande wa kulia, wakati nikitoa wito mwingine. Njoni moja kwa moja huku, mkipenda, njoni upande wa kulia, moja kwa moja hivi. Hebu wafanyakazi wa kibinafsi wawafuate hawa, sasa hivi, sasa hivi, chumbani. Huku, mhudumu na wafanyakazi wa kibinafsi, waje moja kwa moja upande huu chumbani.

Unapowazuru wengine,

201 Ni wangapi wasio na Roho Mtakatifu, ni nani wangetaka kuingia wampokee Roho Mtakatifu sasa? Mlango uko wazi, ingieni pamoja nao, hiyo ndiyo sababu ya wao kuingia. Wameokoka. Wanakuja . . . Mungu aliponena na mioyo yao, nao wakasimama, walikuwa ni uteuzi wa Mungu. Mungu aliwaita. Yesu alisema, “Hakuna mtu angeweza kuja, asipovutwa na Baba Yangu. Wote alionipa Baba, watakuja Kwangu.” Hiyo ni kweli. Kwa hiyo, wameenda chumbani.

202 Mtu mwingine angetaka kuingia pamoja nao kutoka kwenye roshani, ambaye hana Roho Mtakatifu? Tunao wakufunzi, na kadhalika, wanaoweza kuwapa maelekezo, na kukaa hapo siku nzima na usiku kucha mkitaka, mpaka mtakapoupata ubatizo wa Roho Mtakatifu.

203 Ndugu, ni kitu muhimu, huna budi kuuamini, huna budi kuwa nao, la sivyo utaangamia. Ingia, hivi hutaingia, wakati tukiimba mara nyingine tena?

Nikitumainia tu ustahi Wako,
Naomba kuuona uso Wako;
Iponye roho yangu iliyojeruhiwa, iliyovunjika,
Niokoe kwa neema Yako.

Hebu tuinue mikono yetu, kila mtu sasa.

Mwokozi, Mwokozi,
Sikia kilio changu kinyenyekevu;
Unapozuru wengine,
Usipite . . .

204 Baba yetu wa Mbinguni, jalia kusiwe na mmoja miongoni mwetu atakayeachwa. Nimewapa kadiri nijuavyo, Neno Lako, nikilinukuu jinsi tu lilivyoandikwa, akibisha mlangoni, milango ya vyumba vya moyoni, akisema ya kwamba "Atakaye, anaweza kuja na kunywa Maji ya chemchemi za Uzima bure; bila pesa, bila gharama. Njoni tusemezane, ingawa dhambi zenu ni nyekundu sana, zitakuwa nyeupe kama theluji; nyekundu kama bendera, zitakuwa nyeupe kama sufu."

205 Basi unapoangalia kupitia Damu nyekundu ya Mwanao, tunajua ya kwamba nyekundu kupitia nyekundu inaonekana nyeupe, na bila hiyo, ingali ni nyekundu, huko nje chini ya Damu, mbona, hakuna ondoleo la dhambi. Nao wamekuja, wengi wao, kuikubali, Baba. Kuna wengi humu jengoni, sijui mioyo yao, Wewe unaijua, kwamba nitakaposimama, kama Siku ya Hukumu itakuwa leo hii, bado, au kesho, basi hakutakuwako na damu ya mtu yeyote juu yangu, kwa sababu nimekukabidhisha Wewe kwao kwa Neno Lako, naye Roho anasema, "Njoo," Bibi-arusi alisema, "Njoo." "Kila atakaye, aje anywe maji ya chemchemi za Uzima bure."

206 Mungu, jalia ya kwamba hakutakuwako na mtu aliyepotea hapa, ila watakaokuwapo Siku ile, wameokoka na wako chini ya Damu. Huko nyuma chumbani, ambamo hao watenda kazi wanafanya kazi, Mungu, ninaomba ya kwamba utamjaza kila mmoja wao kwa Roho Mtakatifu. Wape shauku ya moyo wao. Tujalie.

207 Jalia wapate ushirika miongoni mwa watakatifu sasa, wawe washiriki wa baadhi ya makanisa haya mazuri katika jamii yao. Wabariki wale wanaotafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu, jalia Yeye aje kwa neema juu ya kila mmoja wao. Tusaidie sasa, tunapoufanyiza mstari wa maombi, waponye wagonjwa na wanaoteseka.

208 Ndipo wakati maisha yamekwisha, Baba, mahubiri ya mwisho yamehubiriwa, ambalo nitafanya siku moja, itabidi maisha yangu yaishe hapa duniani kama Yesu akikawia, halafu basi Biblia yangu ifungwe kwa mara ya mwisho, wimbo wa mwisho umepigwa, basi jalia tukutane na Wewe, Bwana, katika amani. Njoo, Bwana, sasa na ujionyeshe kuwa hai kwetu, tunapokungojea Wewe kwa ajili ya wagonjwa. Katika Jina la Bwana Yesu, tunaomba, kwa ajili ya utukufu Wake. Amina.

209 Sasa, ninaamini Billy alisema aligawa kadi mia moja za maombi. Sijui zingekuwa ni herufi gani. E? Vema,

kusingekuwako na zingine, kwa vyovyote vile, maana tuliombea kila . . . [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

210 . . . dawa itakayokuponya, kama akifanya hivyo, ha—hajui anachozungumzia. Uponyaji ni kuzidishwa kwa seli au uhai. Dawa haitaleta uhai. Kama walikuwa na . . . hebu dawa itengeneze uhai, tungeweza kuimiminia kwenye chupa, na kuitikisa, na mtu atoke. Mnaona? Lakini sisi si . . . Hatuna. Ukienda . . .

211 Sasa, unasema, "Ndugu Branham, maoni yako ni yapi kuhusu madaktari?"

212 Ninaamini wao ni watumishi wa Mungu. Ninaamini ya kwamba kuna wengine miongoni mwao ambao sio, lakini kuna wengine miongoni mwa wahubiri ambao si watumishi wa Mungu, pia. Napata madaktari wengi wanaoamini, kuliko ninavyopata wahubiri wanaoamini, katika mambo ya kimbinguni.

213 Nilitembelea hospitali moja hapa, si muda mrefu uliopita, nikafanyiwe uchunguzi kabla ya kwenda ng'ambo, nikazungumza na madaktari wote, na kila mmoja wa hao wafanyakazi anaamini katika uponyaji wa Kiungu, bila shaka, kama utaliwasilisha kwao kwa busara. Mmoja wa madaktari wakuu katika hospitali fulani hii aliniambia, kasema, "Mbona, Bw. Branham," kasema, "tunawasukuma nyuma watu waliokufa, hawana mapigo ya moyo hata kidogo," kisha kasema, "muda si muda wajua," kasema, "tunatambua chumba hicho cha upasuaji, Mtu fulani yuko mle ndani mbali na sisi." Hiyo ni kweli.

214 Sasa angalieni, vipi kama nikiuvunja mkono wangu, kisha nimwendee daktari na kusema, "Uponye Dak, upesi sana, nataka kumaliza kazi yangu"?

Angesema, "Unahitaji uponyaji wa akili."

215 Hiyo ni kweli. Anaweza kuukarabati, bali Mungu hana budi kuponya. Mungu hana budi kutoa kalisi na kadhalika inayoingia kwenye mfupa huo, na kuunganisha mfupa huo, hakuna dawa itakayofanya hivyo.

216 Sasa, vipi kama nilikuwa na kidole tumbo, kilichombidi daktari kukifanyia upasuaji? Hakuniponya, alitoa tu kidole tumbo. Ni nani atakayepaponya mahali walipokata? Hakuna dawa itakayopaponya.

Mtu fulani aliniambia, kasema, "Ndugu Branham . . . "

217 Wakati mmoja nilitoa tamshi kama hilo, nililisema hivi, nikasema, "Dawa yoyote itakayouponya mkono wangu, kama nikiukata mkono wangu . . . Angalieni, kama nikiukata mkono wangu, ningeanguka chini nife, mngeweza—mngeweza kuweka dawa zote ulimwenguni kwenye mkono wangu, na kuutia mwili wangu dawa usioze kunifanya nionekane wa kawaida

kwa muda wa miaka hamsini, jeraha hilo lingekuwa tu kama lilivyokuwa wakati nilipoanguka chini nikafa." Hakika. Kama dawa inaponya, kwa nini isiponye? Sasa, dawa itakayoponya jeraha mkononi mwangu, itaponya jeraha kwenye koti langu, itaponya jeraha *hapa*.

"Mbona," unasema, "dawa haikutengenezwa kwa ajili ya koti lako wala *hili*."

Vema, vipi kuhusu mwili wangu basi, kama mimi, kama nikianguka chini nife, nawe uushone, na kuutia mwili wangu dawa usioze, kwa nini isiuponye kama inauponya mwili?"

"Kwa nini," unasema, "uhai umetoka."

218 Loo! Jambo ndilo hilo. Uhai. Kwani uhai ni nini? Niambieni uhai ni kitu gani, nami nitawaambia Mungu ni Nani. Kwa kuwa Mungu ni Uzima tele. Kweli kabisa. Ni mtazamo wako kwake. Unaona? Huwezi kufanya hivyo. Kwa hiyo, hu—huna budi kukumbuka hilo, ya kwamba Mungu ndiye Mponyaji pekee aliyepo.

219 Mtu fulani aliniambia wakati mmoja, kasema, "Ndugu Branham, vipi kuhusu penisilini kwa nimonia, mafua makali?"

220 Nikasema, "Hakika. Penisilini ni kama kutia sumu ya panya nyumbani mwako, wakati panya wamekula mashimo nyumbani mwako, inawaua panya, lakini haiponyi hayo mashimo alipokula." Kweli kabisa. Penisilini ni sumu, dawa ya kuua vijidudu, halafu haininii—hairejeshi seli ya damu iliyorarua, Mungu hana budi kufanya hivyo. Bila shaka.

221 Kwa hiyo, Mungu ndiye Mponyaji pekee aliyepo, kama sivyo, Biblia imekosea, Mungu alisema katika Zaburi 103:3, "Mimi ni Bwana niponyaye magonjwa yako yote." Ninashikilia ninii yangu . . .

222 Wakati ni—nilipohojiwa kwenye Kliniki ya Mayo, waliniambia, "Hatuninii . . . " Mzee, Jimmy Mayo katika maskini wale ndugu wa Mayo alikuwa na kitu huko nyuma ofisini, ambapo alikuwa nacho kule, walinirudisha na kunionyesha, wakati huyu Donny Morton . . . Wangapi waliyasoma kwenye *Reader's Digest*? Wakati Mayo ilipomkataa, na kadhalika, naye akaja huko California, huko chini kutoka Canada Bwana alimponya, akampa afya. Nayo Mayos ilikuwa imemkataa, vivyo hivyo na Johns Hopkins, huyo mvulana aliponywa. Nao, nilihojiwa juu ya jambo hilo, nao wakasema, "Hatudai kuwa waponyaji, tunadai tu kuyasaidia maumbile, Mungu ndiye Mponyaji pekee." Sawa.

223 Kwa hiyo, madaktari ni watumishi wa Mungu. Siwezi—si—si—siwezi kuponya, daktari hawezi kuponya. Sasa, yeye hufanya kazi kwa kuondoa kivimbe, ama kung'oa jino bovu; sijishughulishi na uvimbe huo, ninashughulika na uhai katika uvimbe huo, roho, kansa, ni ibilisi. Biblia ilisema, "Wakati

pepo kiziwi na bubu alipomtoka huyo mtu, aliweza kunena na kusikia." Mnaona? Roho.

224 Iwapo—iwapo huyo mtu ni kiziwi na hawezi kusikia, daktari anasema mishipa imekufa. Vema, kwa nini haijakufa kote mwilini mwake? Namna hii tu: Vipi kama kuna mkanda wa uwazi mkononi mwangu ambao ulikatisha mzunguko wa damu? Punde mkono wangu ungekufa, usifae kitu. Vema sasa, hamwezi kuona jambo hilo, daktari hufanya kazi tu kwa hisi mbili, mbili kati ya hisi zake tano: kile anachoweza kuona, kile anachoweza kuhisi. Vema sasa, kama hawezi kuiona ama kuihisi, basi wakati bendi hiyo itakapoachiliwa, ndipo mzunguko utaanza tena. Kama vile tu maumbile . . .

225 Mama mmoja alikuwa na mtoto mwenye kifafa kule, hivi majuzi usiku, katika chumba cha dharura, nami nikamwombea maskini jamaa huyo mdogo, nikamwambia, nikasema, "Kama ubua wa mahindi ukiota, kama usiposumbuliwa na kitu, utazaa ubua wa mahindi, mzuri ulionyoka, suke zuri. Kama kwekwe likijifunga kwake, bonge liwe juu yake, linate, utapinda. Vema, hivyo ndivyo ilivyo kwa kifafa au chochote kile, kuna kitu kinachokizuia. Vema, kama unaweza kuondoa hicho kizuizi, kitu hicho kitakua moja kwa moja."

Sasa, watu wengi husema, "Vema, sioni tofauti yoyote sasa."

226 Hilo halina uhusiano wowote nalo, hata kidogo. Ondoa hilo bonge kwenye huo mhindi, haunyooki sasa hivi, upe tu nafasi, ukikaa kwenye jua lenye joto, mvua, uangalie ukinyooka kabisa. Vivyo hivyo utafanya jambo lile lile, wewe amini tu, ni Mungu. Moja, uhai wote wa nuru hiyo ni uhai wa mimea unaotokea kwa njia ya j-u-a, bali Uzima wa Milele huja kupitia M-w-a-n-a (Hiyo ni kweli?), Mwana wa Mungu.

227 Hebu nikwambie unachoweza kufanya, hebu umimine zege ujiani mwako, weka nyasi chini hapo. Ni wapi ambapo nyasi zako zitakuwa nyingi zaidi kwenye msimu ujao wa kuchipua? Moja kwa moja ukingoni mwa hicho kinjia. Kwa nini? Ni uhai huo mle ndani, huwezi kuuficha uhai. Wakati hilo jua linapoanza kuipasha joto hiyo zege, maskini uhai huo utakua ujitokeze moja kwa moja, moja kwa moja, na kuinua kichwa chake na kumsifu Mungu. Na hiyo ni kweli. Huwezi kuuficha.

228 Hebu chukua m—mmea na kuuweka chini ya birika, upindue hiyo birika juu chini, angalia mmea huo ukipinduka moja kwa moja, na kupanda juu moja kwa moja na kumsifu Mungu. Kweli, huwezi kuuficha uhai. Na wakati Uhai ukiwa moyoni, Mungu yuko moyoni, huwezi kuuficha. Loo, Yeye ni halisi.

229 Sasa, angalieni mstari huo wa watu, umeenda moja kwa moja ukumbini mpaka nje. Vema sasa, mnajua vizuri sana nisingeweza kufanya upambanuzi kote kwenye watu hao, mnaona. Ni wangapi wanaojua hilo? Mbona, yapata baada ya wanne ama watano, ningekuwa karibu kuzimia basi.

230 Ni wangapi humu ndani sasa, vema, hamna kadi zozote za maombi, bali unaamini kwa moyo wako wote ya kwamba Mungu huponya? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . kupona. Vema, sasa nendeni na . . . [Sehemu tupu kwenye kanda.] . . . mnaona, huduma ya kwanza wakati Bwana aliponiambia niwawekee mikono, wangeweka mikono yao juu ya wangu.

231 Njoo hapa. [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . ? . . . Naam, bwana. Sasa, kama nilivyosema hivi punde, chochote kisichokuwa na kijidudu, hakingeonekana, lakini kinaonekana. Una ugonjwa wa tumbo. Unaamini Bwana atakuponya huo? Ninataka uone jambo hili, ninataka uangalie mkono wangu. Sasa ondoa mkono wako. Unaona? Sasa ninauwekelea wangu, haufanyi hivyo. Unaona? Lakini wako . . . Sasa, sehemu ya ajabu: Nilijuaje shida yako? Unaona? Huyo ni—huyo ni Roho Mtakatifu. Sasa unaamini nikikuombea, utaondoka? Kwa moyo wako wote? Uangalie.

232 Baba yetu wa Mbinguni, na ijulikane ya kwamba Wewe ni Mungu, na imeandikwa katika Maandiko, "Katika Jina Langu, watatoa pepo."

233 Ninampa changamoto ibilisi huyu anayemdhuru dada yangu, katika Jina la Yesu Kristo, toka kwake!

234 Sasa, unaangalia, wewe mwenyewe, mama. Sasa, kabla sijafungua macho yangu ama chochote kile, na ndugu pale aliyekuwa akiuangalia mkono wangu, pia, umerudi kuwa wa kawaida, sivyo? Sasa, kuna jambo fulani lililotukia, sivyo? Umeponywa.

Amini tu.

235 Sasa mama huyu, simtazami nipate ono. Weka mkono wako juu ya wangu, mama. Naam, bwana! Ametiwa uvuli wa mauti, kansa. Je, unajua hilo? Sasa, hana budi kupata uponyaji, la sivyo afe. Sasa, si—si—siwezi kulielezea. Mimi—mimi . . . Inakubidi tu kuliamini, hakuna lingine, mimi, hakuna njia kwangu kulifanya. Sasa, mama, kama ningeweza kufanya lolote kukusaidia, ningekuwa mnafiki kama sikufanya hivyo, lakini si—siwezi kufanya zaidi ya kuomba. Kama mimi na wewe tutakubaliana pamoja, kama vile Yesu alivyoahidi katika Biblia, nawe utaamini hili kwa moyo wako wote . . .

236 Unafikirije kwamba ninajua ya kwamba ulikuwa unateseka namna hiyo? Kwa karama. Hiyo ni kweli? Unaamini karama hiyo inatoka kwa Mungu? Sasa, kama tutakubaliana sasa, ninaweza kuufanya ukuache, nawe unaweza kuuona ukiondoka. Lakini kama—kama—kama tutaweka imani yetu pamoja, halafu basi kama ukiondoka, siwezi kusema utadumu, sasa, mnaona, ninashughulika na uvimbe, mnaona, sasa, uhai mle ndani, huo uvimbe labda ungali utakuwako. Lakini baada ya siku chache uvimbe huo utavimba, utakuwa mkubwa zaidi, basi achana tu nao, hauna uhai, basi ni kama mbwa mdogo anayekanyagwa

barabarani, atasinyaa kwa muda, lakini basi atavimba na kuwa maradufu ya ukubwa wake.

237 Watu wengi husema, "Nilipoteza uponyaji wangu."

238 La, hiyo ndiyo ishara uliupata. Ukiwa mgonjwa, ni kipande cha nyama iliyooza kimewekwa pale, moyo hauna budi kuusafisha mkondo wa damu, kwa hiyo unadunda kupitia pale, ndipo maambukizi yanaanza, anashikwa na homa, na kadhalika, hiyo inaonyesha ya kwamba umepata uponyaji wako. Watu wengi husema, "Loo, niliukosa, niliukosa." Mnaona?

239 Sasa, utaamini? Sasa, kumbuka anapotoka, atapitia mahali pasipo maji. Sasa, kama utaamini, weka mkono wako hapa. Ninataka uelewe, kwa hiyo . . . Njoo hapa karibu, kwa sababu uko katika hali mbaya. Nataka uuangalie mkono wangu. Unaona? Sasa, kwa namna fulani unageuka kuwa mwekundu, na vitu vidogo vyeupe vinapitapita juu yake. Sasa, hiyo siyo sehemu ya ajabu. Sasa, chukua mkono wako mwingine hapa, na uuweke hapo, uh-huh. Sasa, haufanyi hivyo hapo, sivyo? Wala haufanyi hivyo juu ya *huu*. Lakini sasa, wekela mkono *huu* juu yake. Unaona, hivyo ndivyo anavyofanya, huyo hapo anaenda. Unaona?

240 Sasa, kama tutakubaliana . . . Kuonyesha ya kwamba Mungu hutimiza Neno Lake, hii hapa ishara ya kimwili. Nauweka mkono wangu chini namna *hii*, ili kwamba upate kuona haujasogezwa. Vema. Sasa, unaona jinsi tu unavyoonekana?

241 Sasa, ninataka kila mtu uendelee kuinamisha kichwa chako, kwa sababu huku ni kumtoa pepo mchafu. Na wakati anapokasirika na inambidi kulazimishwa kutoka . . . Kwa kawaida ninamwachia mgonjwa, kama wanataka kuamini, vema, nimefanya yote niwezayo kufanya, wakati huu, ili kwamba kusanyiko, mtu huyu, wahudumu, wowote wale, wapate kuliona, na kujua ya kwamba limetendeka, huyu mwanamke akiangalia pale, vema basi, Mungu na awe mwamuzi. Sasa iweni na kicho. Na mnapoangalia, angalieni mkono wangu.

242 Bwana, huyu mwanamke anauangalia mkono wangu, anajua ya kwamba kitu Fulani cha kisiri kilijua shida yake. Ninakuomba, Baba, katika Jina la Kristo, ya kwamba hutamwajibisha na hili, bali tunawataka watu wajue ya kwamba Wewe unabisha milango, naye anaangalia athari hii ya kimwili hapa. Nami ninakuomba, Wewe, Baba, ya kwamba utamfanya atoke mwilini mwake. Nisikie, Baba, katika Jina la Kristo.

243 Sasa bado, hajaondoka. Sasa, huyu mama ni shahidi, anaangalia. Ningali ninauhisi, karibu unaupoozesha tu mkono wangu. Sasa iweni na kicho, kila mtu; sijafungua macho yangu bado.

244 Shetani, sayansi ya tiba inakuita *kansa*, ambalo linamaanisha "kaa," bali tunakujua kama ibilisi, mwuaji, mauti, wala mauti na uhai haviwezi kuishi pamoja. Ninakuja

katika Jina la Yesu Kristo, nikileta uzima. Toka ndani yake, ninakuamuru, katika Jina la Yesu, mwache!

245 Sasa hebu huyu mama awe mwamuzi. Sijawahi kuusogeza mkono wangu, bali ameondoka. Hiyo ni kweli? Sasa inua kichwa chako. Sasa, huku mkono wangu ukiwa juu ya meza hii hapa, huyu mama ndiye shahidi. Sasa angalia, mama, ili upate kuona. Sio hivyo, sivyo? Sio hivyo, sivyo? Sasa chukua mkono huu. Unaona? [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

Katika Jina la Yesu, huyu mtoto mdogo na aponywe.

Kama tu utaamini. . .[Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . .?. . .

246 Ilionekana kana kwamba kusanyiko lote linachanua sasa kwa. . .Kwa nini hamkufanya hivi mwanzoni? Wote wanaougua shinikizo la damu, simameni kwa miguu yenu huko nje, anemia, na kadhalika, kisukari, ama chochote kile, simama kwa miguu yako na uamini kwa moyo wako wote, kila mahali, mahali popote, orofani, huku chini, popote pale. Nitawaitaje? Mnaona? Endeleeni kusimama.

Simama hapa kwa dakika moja tu.

Njoo, ukiamini. Njoo hapa, papa hapa. Angalia hapa, dada, kisukari. Nanyi simameni papa hapa, pia.

247 Wagonjwa wote wa kisukari simameni kwa miguu yenu, mtaona jambo fulani likitukia sasa, kama tu mtaamini. Iweni na imani. Aminini kwa mioyo yenu yote. Vema. Unaamini kwa moyo wako wote?

Katika Jina la Bwana Yesu, ndugu yangu na aponywe. Amina.

Bila shaka, wewe ni kiwete, huo ni ugonjwa wa yabisi kavu. Simama hapa.

248 Kila mtu aliye na yabisi kavu simama kwa miguu yako. Angalieni hapa. Mnaona?

249 Vema, njoo, dada, papa hapa. Niangalie huku, unaniamini mimi kuwa ni mtumishi wa Mungu? Nimejua tangu umekuwa ukiketi hapo ukifurahia uponyaji huo ya kwamba ulikuwa na hiyo pumu, lakini unaamini ya kwamba Mungu atakuacha uiondokee? Naam.

250 Kila mtu aliye na pumu, simama kwa miguu yako, simama tu. Kama Mungu anaweza kumponya mmoja hapa, anaweza kuwaponya huko nje, sivyo? Ugonjwa wa pumu.

Vema, ugonjwa wa figo.

251 Vema, wote walio na ugonjwa wa figo simameni kwa miguu yenu. Vema. Amini kwa moyo wako wote.

Njoo hapa, dada, niangalie, ugonjwa wa tumbo, simama papa hapa.

252 Wote walio na ugonjwa wa tumbo wasimame. Vema. Niangalieni hapa.

Loo, kusanyiko lote linasumbuliwa na shida yako, wasiwasi.

253 Kila mtu aliye na wasiwasi, simama kwa miguu yako. Kila mtu aliye na wasiwasi, simama kwa miguu yako.

254 Angalieni hapo, ningewezaje kupitia kwenye kusanyiko hilo nikiwaita watu hao wote? Lakini Roho Mtakatifu, Yuko hapa ndani, kuna mengi sana yanayokuja kwa wakati mmoja, siwezi kujua Yuko wapi.

255 Loo, Yeye anabisha. [Ndugu Branham anagongagonga mimbarani—Mh.] Mnaamini hilo? Huu ndio wakati, hii ndiyo saa. Kila mtu aliye mgonjwa, simama kwa miguu yako, kila mtu anayetaka kuponywa, simama kwa miguu yako na uinue mikono yako.

Njoo, dada, wasiwasi umekwisha . . .?. . . Nenda, amini.

Inueni mikono yenu. Je, mnamkubali Kristo kama Mponyaji wenu? Endapo mnamkubali, mpungieni mikono yenu.

256 Ee Mungu, Mwanzilishi wa uzima, Mpaji wa vipawa vyote vyema, tuma baraka Zako juu ya watu hawa, ambao ninawabariki katika Jina Lako.

257 Shetani, umeshindwa vita, umefichuliwa, umati huu unajua ya kwamba umefichuliwa. Wewe ni ibilisi, wewe ni mwongo, wewe ni laghai, nasi tunaufichua udanganyifu wako Mbele za Roho Mtakatifu. Kama mtumishi wa Mungu, pamoja na karama ya uponyaji iliyohudumiwa na Malaika anayekufichua, toka ndani yao, Shetani, katika Jina la Yesu Kristo!

258 Inueni mikono yenu na kumpa Yeye sifa, nami nitawahakikishia uponyaji wenu, kundi lote lenu, katika Jina la Yesu Kristo. Mungu awabariki.

60-0803 Ibrahimu
Eisenhower High School
Yakima, Washington Marekani

SWAHILI

©2025 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org